# Yehova-Yire #2

Grass Valley, California, Amerika
Julai 06, 1962

1 1Asante, Ndugu Roy. Hebu tubakie tukiwa tumesimama kwa kitambo kidogo tu tunapoomba. Tuinamishe vichwa vyetu, kama mtaweza. Na hebu tuwazie tu sasa kama kuna chochote moyoni mwenu ambacho mngetamani Mungu awajibu, jioni hii, hitaji fulani, hebu liachie tu hilo lijulikane unapoinua mkono wako, na useme, "Ninalo hitaji mbele za Mungu." Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu tunapoomba.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunaichukulia hii tunu kuu, kuja Kwako; tukijua hili, kwamba kama tukija katika Jina la Bwana Yesu, tumeahidiwa kuwa tungelipokea kile tunachokiomba. Sasa hatuji kwenye Kiti Chako cha Enzi cha Hukumu. Kwa kweli tusingetaka kuja pale, au kwennye Kiti cha Enzi cha Haki. Lakini sisi…tunakuja kwenye Kiti cha Enzi cha Rehema, pale ambapo tuna-tuna hakika kujaliwa mahitaji yetu. Kwani, tusingehimili hukumu Yako, wala kuweza sisi kuishi kwa haki Yako, bali rehema Zako ndiyo tuombayo. Tusamehe basi, Bwana, dhambi zetu. Tunaomba kwamba utatulia hilo, na kwamba Wewe utakuwa pamoja nasi jioni hii, ukijibu kila hitaji ambalo hiyo mikono iliwakilisha ilipoinuliwa juu. Ulijua ni nini kilicho chini ya huo mkono, ndani ya moyo. Na, Mungu, hapana shaka ilikuwa ni kwa ajili ya ugonjwa, na wokovu, na wapendwa. Tunaomba jioni hii, Baba, hasa kwa ajili ya hao, kwamba utawajalia mahitaji yao.

3 Sasa tumekuwa tukiongea juu ya mtumishi Wako mtiifu, Abrahamu, tukiendelea naye jioni hii, katika safari yake. Tunaomba kuwa utatubariki tunapoendelea chini njiani mwa miaka mamia mengi iliyopita, tukiwa na mtumishi mwaminifu aliyeamini Neno Lako. Hebu hilo liwe mfano, kama Paulo alivyosema katika Waebrania, kwa kile Abrahamu alichokuwa, mfano. Na tunaomba kwamba yeye, ile imani yeye aliyokuwa nayo, itafunuliwa kwetu jioni hii; tuamini Neno la Mungu, na hapana shaka juu Yake, Neno moja la Hilo, bali tuliamini Hilo lote, na tuamini kila kitu Yeye alichosema. Na hebu sisi tuweze kushikilia hizo ahadi ambazo Yeye alifanya kwa ajili yetu, na tuwe watoto wa Abrahamu kwa kuwa ndani ya Kristo. Tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina. Kaeni.

4 Ndugu Borders ni mrefu zaidi kidogo kuliko mimi, hivyo inanipasa kushusha kipasa sauti chini zaidi kidogo. Na ni tunu kuwa hapa jioni hii katika huu mkutano tena, na kuombea wagonjwa, na kufanya chochote kile Roho Mtakatifu anachotupa sisi tufanye. Nataka kusema hili, maelezo ya sifa njema. Ya safari zangu zote katika Amerika, Amerika na Canada, niliona kitu fulani jioni iliyopita kilichonisisimua zaidi ya viti vyote vyenye magurudumu nilivyowahi kuona vikiachwa na watu, na magongo yote ya kutembelea yaliyowekwa chini, vipofu kuona, viziwi kusikia; bubu kuongea, wafu walifufuliwa, daktari alitia sahihi taarifa kuwa "yule mtu alikuwa amekufa, na kufufuka." Hilo ndilo lote limekuwa likisisimua. Lakini nilipoona watu jioni iliyopita, ambao ni washirika wa kanisa, wakipokea Kweli na kusimama moja kwa moja katikati ya hao watu, ili kuungama makosa yao na wakitaka kufanya lililo sahihi, hilo lilikuwa bora zaidi ya yote ninayoyajua.

5 Kanisa, labda Bibiarusi amekwishachaguliwa. Hilo ni, kumwandaa Buibiarusi kuwa tayari sasa. Kumfanya Bibiarusi…

Uamsho umekwisha. Tunajua hilo. Hakuna roho ya uamsho tena.Saa mbili za ibada, kila mtu analalamika. Katika uamsho, ni mchana na usiku, wakati wote, kamwe hakuna kusitisha. Uamsho umekwisha. Na hivyo tunaokoteza shambani tu.

Ilimpasa Abrahamu alitolee hilo jasho hadi yeye akampata yule mtu wa kipekee. Na ndipo wakati yeye alipompata huyo mtu wa kipekee, kitu kilichofuata ilikuwa kumwandaa bibiarusi basi ili akutane na bwana arusi. Hicho ndicho kitu kilichofuata. Unakumbuka yeye alipompata? Katika wakati wa jioni, ile nuru ya jioni.

Kilichowavutia wanawake na mwanamume, wote wawili, jioni iliyopita; na kuwaona, kulingana na Neno, wakisimama na kukubali wao wana makosa, wakitaka msamaha wa Mungu, na kuendelea mbele. Hapa ni mahali pa kuwa na uamsho. Kama kungekuweko na uamsho wowote ninaoujua, huo umetukia papa hapa, palipo na mioyo mikunjufu. Kwa nini? Unacho kitu fulani cha kutendea kazi, unaona. Kitu fulani…Wengi wao watakuwa wajeuri, wao hawataki uwaambie juu ya hilo; kumbuka tu, uzao wa aina hiyo ni uzao wa kidhehebu, siyo Uzao wa Abrahamu. Uzao wa Abrahamu unaliona Neno, nao unaliamini Neno, kwa haraka.

6 Wakati yule kahaba mdogo, pale kisimani jioni ile, yule mwanamke pale kisimani…Kulikuweko na makuhani na walimu wakiwa wamesimama pale, wakimtazama Yesu akitenda, akitoa ishara Yake ya Kimasihi kwao, ishara ya Kimaandiko, nao walisema, "Yeye ni Beelzebuli, pepo, mpiga ramli."

Lakini mara ile Nuru ilipommulika yule mwanamke mdogo, wakati Yeye alipomwambia kile yeye alichokwishafanya, yeye alisema, "Bwana, natambua ya kuwa Wewe ni Nabii. Na sisi tunajua kuwa Masihi anakuja, na Yeye atakapokuja, Yeye atatuambia hayo mambo." Unaona, kwa haraka ile Mbegu iliyochaguliwa tangu asili ilidaka hilo, kwa sababu hiyo ilikuwa Mbegu ya Abrahamu, kwa kweli. Na yeye aliona ile Nuru. Hiyo ilikuwa ni Neno. Yeye alijua kuwa Neno liliahidi hiyo, Masihi atakapokuja, Yeye angelifanya hayo mambo, na yeye alitambua hilo.

Yesu alisema, "Mimi Ndiye ninayenena na wewe."

Huyo mwanamke alikimbilia mjini na kujaribu kushawishi wengine. Yeye alisema, "Njooni, mumwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyokwishafanya. Je, huyu siye yule Masihi?" Unaona?

7 Sasa neno tu kwa dada zetu. Siku zote nimechukuliwa kama anayemchukia mwanamke, lakini sivyo nilivyo. Unaona? Mimi nilipokuwa mtoto mdogo, nilipitia machungu; lakini siku zote nimekuwa na heshima kuu kwa mwanamke ambaye alikuwa mwanamake, bibiye. Lakini sijawa na heshima kwa hao wanaokiri kuwa hivyo na hawako hivyo. Napenda kumwona bibiye, bibiye halisi hasa, yeye ni jiwe la thamani.

Katika siku hii wakati wanawake wamepotoka, wengi wamepotoka katika hizi siku za mwisho. Andiko linasema hivyo. Kwa nini? Huko ni kuondoka kwenye kipindi. Unakumbuka upotofu wa kwanza ulikuwa nini? Ulikuwa ni mwanamke. Hilo ni sahihi. Na katika siku ya mwisho! Kamwe hatukuwahi kuwa na hili; tumekwishakuwa na miaka elfu sita ambayo akina bibiye walijaribu kubakia kuwa akina bibiye. Sasa wanajaribu kutenda kama mwanamume, wanavaa nguo kama mwanamume, wanakata nywele zao kama mwanamume, na kadhalika. Kamwe hawakuwahi kufanya hilo katika kipindi kingine chochote. Biblia inabashiri hili, kuwa wao wangelifanya hili katika siku za mwisho. Na mpo hapa, upotoshaji wa wanawake. Si ajabu Biblia ilisema, "Hao waliotoroka kutoka-kutoka-kutoka Sayuni watatukuzwa mbele za Bwana, katika siku ile." Unaona, jinsi ambavyo hao walitoroka!

8 Unasema, "Hilo halifanyi tofauti yoyote." Hilo linafanya tofauti. Mtu fulani aliniambia siyo muda mrefu uliopita, akasema, "Ndugu Branham, hicho kitu kidogo hakifanyi tofauti yoyote."

Nikasema, "Hilo lilifanya kwa Paulo. Na Paulo alisema, 'Kama malaika kutoka Mbinguni akija na kufundisha chochote kingine, hebu yeye na alaaniwe.' Ama wawe mhudumu, au malaika, au askofu, papa, au chochote kile yeye alicho, hebu yeye na alaaniwe kama kitu chochote kiko kinyume na Hili.'" Unaona, ni hivyo kabisa. Wagalatia 1:8, kama unataka kusoma Hilo.

Na yeye akasema, "Vema, mimi sifikiri…" Kasema, "Nimewaona wanawake wakiwa na nywele fupi, walikuwa tu wanyenyekevu na wazuri."

Nikasema, "Hilo ni sahihi kabisa, mimi nimeona hilo pia. Lakini hilo silo. Unaona, inakupasa uje kwenye kile Biblia ilichosema."

Vipi kama Mungu alimwambia Musa, "Vua viatu vyako," na yeye aseme, "Bwana, nitaondoa tu kofia yangu, badala ya hilo"? Unaona? Inakupasa kufanya kile Mungu anachosema ufanye! Na tatizo la hilo, ninaloliwazia, kinachonifanya mimi niwe na hofu mno juu ya hilo, kwamba wahudumu kukivumilia na kitu kama hiki! Hicho ni kitu gani? Hilo linaonyesha ni Adamu wa kisasa aliyekwenda pamoja na mke wake. Unaona? Mungu anahitaji Adamu mwingine anayesimama na Neno, na Yeye pekee, Neno pekee. Neno liko sahihi, hata hivyo! Usiendee njia hiyo.

9 Katika miaka elfu sita, kamwe hapajawahi kuweko na wanawake waliowahi kutamani kukata nywele zao, wavae kama mwanamume, waliopotoshwa. Tuko katika wakati wa mwisho. Na Amerika, mtu yeyote anayejua unabii, anajua kuwa Amerika inawakilishwa na mwanamke. Hii inaitwa "uhuru wa wanawake." Uhuru kwa ajili ya nini? Ili kufanya kama yeye anavyotaka, dhambi.

Mwanamke hawezi kufanya kile yeye anachotaka kufanya. Biblia inasema sivyo.

Mwanamke ni zao la ziada la mwanamume. Yeye hata hayuko katika uumbaji wa kwanza. Hilo ni sahihi kabisa. Yeye alitwaliwa kutoka kwa mwanamume. Mwanamume alikuwa yote mawili hali ya kike na hali ya kiume, Yeye alichukua ile roho ya hali ya kike na kuiweka hiyo katika ubavu uliotoka ubavuni mwake mwanamume. Sikiliza! Je, uliwahi kuona wakati Rebeka alipokwenda kukutana na Isaka, wakati yeye aliporuka kutoka kwenye ngamia, yeye alifunika uso wake kwa shela? Kwa nini? Yeye alikuwa anakuja kwenye kichwa chake.

Wao hawajui hilo. Inawapasa wafanye hilo, hata hivyo. Je, ulimwona mwanamke wakati anapoolewa, yeye huweka shela juu ya uso wake? Kwa nini? Yeye anakuja kwenye kichwa chake. Na Kanisa, Kanisa, likiwa Bibiarusi, inapasa lijifunike kwa shela lenyewe mbali na kanuni yoyote ya dini, hilo linakuja kwenye Kichwa chake, Yeye Neno. Kristo Ndiye Neno, na Yeye ndiye Kichwa.

10 Sasa, marafiki, mimi sitaki nianze kwenye hilo. Mimi-mimi-mimi nilikuwa nikitazama kule leo, nikiwa na maandishi mia tano, maandiko zaidi kidogo ya mia tano ya mafundisho ya kilindi kwenye Biblia. Lakini nataka tu kukaa na Abrahamu kwa huu mkutano, kwa namna fulani.

Unajua, naamini Bwana anaweza, kama ndugu hawatajali, na kama kila mtu, ningelipenda nirejee hapa na kuwa na uamsho ambapo mngeweza kukaa kwa kitambo kidogo, unaona, pale ambapo tungefikia kina hasa na tuone tu. [Kusanyiko linashangilia-Mh.] Asante. Ndiyo. Asante. Asante. Asante. Najua kuna samaki hapa. Mimi-mimi-mimi najua hilo. Na napenda samaki. Na mnayo mali ghafi ya kufanyia kazi, mtu fulani ambaye ni mkweli. Mtu yeyote anaweza kukosea. Ninyi hamjui; mimi hufa kila siku, kutokana na makosa yangu, na kujaribu kuishi mbele za Kristo. Na mtu yeyote ambaye ni mkubwa vya kutosha, na anaye Roho wa Mungu vya kutosha kutembea na kukubali wamekosea, useme, "Mimi nataka kitu kilicho sahihi," ninao ujasiri mwingi mno pale pale, kwani, huo ni Uzao wa kweli wa Abrahamu. Wao wanataka kujua Hilo. Wao hawajui Hilo isipokuwa wao wasikie Hilo. Lakini inapasa hilo lisikike kwanza, unasema, "Tuna…pasipo mhubiri? Na je, mhubiri anawezaje kuhubiri asipotumwa na Mungu?" Hiyo ndiyo ile Kweli kabisa.

11 Sasa, angalia sasa.

Tunarejea kwa Abrahamu sasa. Ni bora turudi nyuma juu yake, hivyo, na tulichukue hilo na kuendelea. Je, mnaweza kunisikia vizuri, juu katika roshani juu pale? Tuna … Ni vizuri kuona, jioni hii, kundi zuri kama hili. Ninyi ni watu wazuri mno hapa. Hakika mimi…

Nilikuwa nikizungumza na rafiki leo, anayetokea Canada. Bwana alikuwa ameniongoza chini kwenda mahali fulani ambapo ilinipasa kutazamia kitu fulani kitukie. Na ndipo nikiwa nimesimama … Huyu rafiki, nilikutana naye, na yeye alikuwa anazungumza juu ya jinsi Waamerika walivyo wema. Na mimi nikasema, "Ndiyo, na ndani hapa, kuna baadhi ya Uzao wa Mungu uliochaguliwa tangu asili, ndani na kote sehemu hizi, na katika hii sehemu iliyo ovu mno." Simaanishi jiji lenu hapa. Jiji langu, kule ninakotokea, ni ovu kama lenu. Lakini ulimwengu wote ni mwovu, lakini uhuni wote umeelea kwenda Magharibi. Tunajua hilo.Ustaarabu umesafiri na hilo. Na pale ustaarabu ulipo, hapo ndipo dhambi inajiimarisha ndani. Hilo ni sahihi. Utazame huo juu na chini hapa. Hili ni eneo la makaburini la mhubiri. Hilo ni sahihi. Utazame Los Angeles, kila kitu na kila mfumo wa dini hutua moja kwa moja ndani mle, na kila mtu anayo kanuni ya imani ya dini, fundisho la dini. Ili kupeleka Neno ndani pale, huwezi kufanya hilo. Umenajisiwa mno! Hilo ni sahihi. Mapepo, mashetani, pale pale kwenye kiti cha Shetani! Lakini bado katikati ya hilo lote, kuna Uzao fulani ndani pale. Na kitu pekee uwezacho kufanya ni kutawanya Nuru. Na kama yoyote ya hiyo Nuru…Kama kuna Uzao pale, utakuja kwenye Uzima mara tu ile nuru itakapoigonga. Inakupasa tu wewe uoteshe Nuru, hivyo tu. Na Yeye ni Nuru ya jioni, tunajua hilo, Neno Lake.

12 Sasa, jioni iliyopita tulimwacha Abrahamu. Nilianza kwenye-kwenye ile sura ya 22, lakini kamwe sikuimaliza hiyo, kwa sababu nilikwenda kuweka msingi juu ya kile Abrahamu alichokuwa hapo mwanzo. Na tulimwacha yeye jioni iliyopita pale Mungu alipokuwa akilithibitisha lile Agano pamoja naye. Ee, nalipenda hilo. Hali akimega mkate, akifanya ahadi na Abrahamu. Na jinsi tulivyofikia…Wakati Yeye alipomwita Abrahamu, na alikuwa anakwenda kulithibitisha hilo agano kwake, Yeye alimwambia Abrahamu achukue wanyama watatu wenye umri wa miaka mitatu, na kuwatenganisha vipande

viwili viwili. Na tulikuwa nao watatu watatu. Hatuna wakati wa kuingia katika hilo. Jamani, unaweza kukaa na hilo, hilo somo moja pale pale, hadi asubuhi, usingeweza kulielezea hilo. Lakini unakuwa tu na namna ya kugonga sehemu za juu juu, na ukitegemea Roho Mtakatifu katika wakati huu afunue hayo mengine ya hilo.

13 Sasa, jinsi gani huo ukamilifu, Dhabihu kamilifu, kamilifu, Mungu alikamilisha katika maisha ya mwanadamu kile Yeye alichokuwa anakwenda kufanya. Tunajua tuna… Tulikuwa na Mungu Baba, ambaye alikuwa Yehova Mwenyenzi. Halafu Huyo alikuwa katika Nguzo ya Nuru, akawachukua Israeli kupitia jangwani. Na Yehova huyo huyo akafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, katika umbo la Mwana pekee, akaumba Hekalu kwa ajili Yake Mwenyewe ili kukaa ndani, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Ule utimilifu wa Uungu kimwili ulikaa ndani Yake, udhihirisho mkamilifu. Ndipo (kupitia lile agano) ile sehemu Yake ya kibinadamu iliondolewa, ilitengwa, kwamba Yeye aweze (hili agano) kutenganisha huo Mwili uliokufa, hiyo Damu iliyomwagika kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na kuufanya Huo na kuuweka penye mkono Wake wa kuume, na akamtuma Roho penye Siku ya Pentekoste. Na Uzima huo huo ulioishi ndani ya Kristo Yesu unapasa uishi ndani ya watu wa agano, Uzima ule ule ukitenda kitu kile kile. Yesu alisema katika Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, matendo niyatendayo naye atayatenda pia." Sasa, ama hilo ni sahihi au ni makosa. Inapasa liwe sahihi! Kwangu mimi, kila Neno la Hilo ni sahihi. Kila Neno ni sahihi kikamilifu. Angalia jinsi Mungu anavyotenda kazi kwa utukufu.

14 Na ndipo jinsi kwamba hao walio wa Baba … kama Mathayo alivyosema, "Kwa hiyo enendeni, mkifundisha mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Unaona? Sasa, Baba…Haimaanishi hatuna Mungu watatu. Tunaye Mungu mmoja katika ofisi tatu. (Hali ya Ubaba, hali ya Uana, Roho Mtakatifu), Mungu yule yule jana, leo na hata milele na milele. Hivyo kabisa.

Sasa angalia hilo lilivyodhihirishwa kwa utukufu kwa Abrahamu, na jinsi kwamba Mungu, katika hii Nuru, alikwenda katikati ya hivi vipande, akivitenga. Kama tu ile…Tulichukua jioni iliyopita, jinsi wao walivyoweka mkataba, waliliandika halafu wakairarua, kwamba lazima walilinganishe. Ule mkataba lazima ulingane.

15 Sasa mnaona, marafiki, hilo ndilo ninalojaribu kusema. Hata miongoni mwa watu wetu wa Kipentekoste, kunafanyika huyu Shetani wa kutumia akili, kujaribu kuwafanya watu … Sasa, mimi naamini katika karama zote za Mungu. Naamini katika kupiga kelele. Naamini katika kunena kwa lugha. Naamini katika mambo yote ambayo Mungu alisema. Lakini bado huwezi kutegemea juu ya lolote la hayo mambo kuwa ndiyo sababu unaye Roho Mtakatifu. Unaona, uzima wako utaendana na hilo. Unaona? Yako… "Kwa matunda yako unajulikana." Unaona? Na hayo ni mambo yanayoniogopesha mimi leo, kwa sababu naona kanisa langu mwenyewe, kanisa la Kipentekoste, likifanyika huo "mfano wa utauwa," likienda mbali na ile Kweli. Na ukileta ile Kweli ya Neno kwao, wanaionea haya Hiyo. Halafu wahitaji, "Njooni, ketini pamoja nami," wao hawatafanya hilo. Unaona, hilo linaonyesha kuna jambo fulani la makosa. Hilo ni jambo linalonitia wasiwasi mimi. Na, sasa, siyo kama mimi niko kinyume na kanisa langu. Nina…

16 Kama mimi ninampenda Kristo, hilo lingekuwa bora zaidi mno kwangu kujivunia Kanisa Lake kuliko ambavyo ingekuwa kumjivunia Yeye. Kwa sababu ni bora wewe ujivunie watoto wangu kuliko kunijivunia mimi. Na, kumbuka, siku zote nimewaza, kama nilikuwa na matone mawili ya ile ile hasa Damu ya Yesu ndani ya kifaa cha kuchajia, ningeishikilia Hiyo iliyoje, kwamba nisiimwage Hiyo. Ningelitembea kwa uangalifu hasa. Lakini jioni hii ninalo kuu kuliko hilo, mbele Zake, ninao walionunuliwa kwa Damu Yake. Unaona, Yeye alimwaga Damu Yake kwa ajili yako. Na hapa mimi ni mhudumu jioni hii, nikishikilia, au nikikuelekeza wewe kwenye mwisho wako wa Milele. Hivyo sitakwenda kunukuu kanuni yoyote ya imani ya dini au amri ya sharti la kanisa; inapasa liwe Neno, kwa sababu hicho ndicho kitu kinachokwenda kudumu. Imani yangu imejengwa juu ya Neno, basi Neno limedhihirishwa hapa hapa miongoni mwetu. Unaona, inapasa iwe!

17 Sasa, kwa hiyo, mimi naamini kuwa Mungu wa Agano la Kale, yote yale Yeye aliyokuwa, Yeye aliyamwaga ndani ya Yesu Mwana Wake. Na yote yale Yesu wa Agano Jipya aliyokuwa, Yeye aliyamimina ndani ya Kanisa lile alilolinunua kwa Damu Yake Mwenyewe. Unaona? Bado kitambo kidogo na kawaida ya ulimwengu huu,‟ kosmos pale, utaratibu wa ulimwengu, "hautaniona Mimi tena. Bado ninyi mtaniona Mimi,‟ ninyi, Kanisa, "kwani nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu.‟ Ndipo ule Uzima, ule Mkataba, yule Roho aliyeondolewa ndani ya Kristo pale Kalvari,

anarejeshwa na kumwagwa juu ya watu, ule Uzao wa Abrahamu, ule ambao Mungu aliufanyia ahadi. Kumbuka, hiyo haikuwa kwa zao zote, bali ule ″Uzao.‟

18 Sasa, kuna fundisho la kuchaguliwa tangu asili ambalo limeoza, upuuzi. Lakini kwa kweli kuna kuchaguliwa tangu asili kwa kweli. Mungu, kwa kujua hapo mwanzo, aliweza kuchagua tangu asili kwa sababu Yeye anao ujuzi wa tangu mwanzo. Mungu hapendi kuwa yeyote apotee, bali, Yeye akiwa Mungu asiye na ukomo, alijua hao ambao wangelipotea na hao ambao wasingepotea.

Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema kabla ya Isaka au-au … kabla ya Yakobo au Esau hajazaliwa, Yeye alimchukia Esau na akampenda Yakobo. Kujua Kwake tangu asili kulimruhusu Yeye ajue kuwa Esau alikuwa mwongo, na Yeye alimwacha Yeye ajue kuwa Yakobo aliheshimu hiyo haki ya kuzaliwa; pasipo kujali yeye aliipataje hiyo, yeye aliitaka hiyo. Sasa, wavulana wote wawili, mapacha, waliozaliwa kutoka kwa mama wale wale mama na baba watakatifu, lakini mmoja alikuwa mwasi na yule mwingine alikuwa mwamini. Sasa Mungu, kwa kuja Kwake tangu asili, alijua hilo.

19 Sasa, Mungu, kwa kujua Kwake tangu asili, Yeye-Yeye haweki shughulki Zake kama…Wewe usingelifanya shughuli zako namna hiyo, kwenye daftari ambalo kurasa zake hazikuunganishwa kama hicho. Mungu alijua, kwa kujua Kwake tangu asili, ni nani angeokolewa, hivyo Yeye alimtuma Yesu ili kuwadaka hao ambao Yeye aliwajua tangu asili kuwa wangeliokolewa. Soma Waefeso, ile sura ya 1, nawe utaliona hilo. Unaona? Sasa, pale.

Ndipo Yeye anatuma chini Injili Yake na kuipandikiza Hiyo, anamtuma chini Roho Wake ili kuifanya Hiyo iwe hai. Sasa, vyote vitakua katika shamba lile lile, Waebrania 6 inatuambia kuwa, "Kwamba mvua huja mara kwa mara," Yesu alisema, "juu ya nchi," na unaona ndani pale, "ili kuandaa, ili kuivalisha vazi nchi; lakini miiba na michongoma, ambavyo vinakaribia kukataliwa, ambavyo mwisho wake ni kuteketezwa." Umelipata hilo? Sasa kumbuka.

20 Tutachukua shamba la ngano. Ninyi watu mnaolima ngano hapa. Na hapa ukame unakuja. Hapa kuna mitambaazi au magugu mliyo nayo hapa, gugu fulani linalofahamika likiwa linakua katika shamba; hiyo mitambaazi katika shamba, yale manyasi yenye utomvu wa rangi ya maziwa katika gurudumu … shamba, michongoma katika shamba. Na ngano iko shambani. Vyote viwili vina kiu. Na mvua inakuja siyo kwa ajili ya gugu, bali kwa ajili ya ngano, lakini hilo gugu dogo litasimama wima na kushangilia kama tu ambavyo ngano itashangilia.

Lakini kwa matunda yao unajulikana. Roho yule yule hushuka juu ya mnafiki na yeye atapiga kelele na msukosuko kama hao wengine, lakini maisha yake ndiyo yanayothibitisha kile yeye alicho. Unaona? Na tunategemea mno juu ya msisimko. Na leo hii shamba limejaa aina zote za misisimko, kila aina ya msisimko usio wa Kimaandiko na kila kitu kingine. Hakika. Lakini inatupasa kurejea kwenye Neno, ile Kweli ya Neno. Lile Neno, kile Hilo lilichosema.

21 Sasa, Mungu akimwambia Abrahamu kuwa kupitia yeye, lile agano la tatu, na agano pekee. Yeye alikuwa tu uthibitisho wa hilo agano ambalo Yeye alilifanya na Abrahamu, ule Uzao wa kifalme, Uzao wa Roho.

Na kwenu ninyi marafiki zangu wa thamani wa Katoliki, mnaposema, "Salamu, Maria, mama wa Mungu," je, hamwoni aibu? Maria anawezaje kuwa mama wa Mungu? Yeye hangeweza. Mnasema, vema…

Nilikuwa nikiongea na mtu fulani siku ile nyingine, wao wanatofautiana. Wao walisema kuwa-kuwa Yesu alikuwa ule-ule uzao wa-wa Maria. Kama Yeye alikuwa uzao wa Maria; kabla ile mbegu haijaja chini kupitia ule mrija, ilipasa pawepo msisimko wa kuleta huo. Basi unamfanya Yehova…Je, mnaona kile mnachofanya Yeye atende?

Mungu, Muumba, aliumba vyote viwili yai na chembechembe ya Damu, na kuleta Hekalu. Na mwanadamu hahusiki na lolote na Hilo. Ilikuwa ni Mungu pekee! Hilo ni sahihi.

Yeye alikuwa mwanamke mwema, hakika. Kuna wema wengi walioketi hapa jioni hii. Na Mungu anapomaliza kukitumia kitu chochote, hicho kinaondoka kwenye sehemu ya tukio. Na yeye siyo mpatanishi. Yeye siyo mama wa Mungu. Yeye ni mwanamke mwema, aliyekuwa mtakatifu Utukufuni, kwa sababu yeye alitimiza kusudi la Mungu. Na kila mwanamke ndani hapa anayo nafasi ile ile, labda siyo kwa njia ile ile, bali

kumtumikia Mungu. Unaona? Mungu atakutumia wewe.

22 Yeye Mungu alimtumia tu Maria kama kiangulio, lakini yule Mtoto alikuwa Mungu. Naam. Yeye alikuwa Muumba wa vyote viwili yai na damu nyekundu. Na damu nyekundu, bila shaka, hutoka kwa jinsi ya kiume, na Yeye alikuwa Muumba wa hiyo. Na Maria alimleta huyu Mtoto pasipo na msisimko wowote, hakuna zaidi ya Roho Mtakatifu akimzinga kwa kivuli huyo mwanamke na kuumba ndani ya tumbo lake la uzazi hii chembechembe ya Damu na yai lililoleta yule Mtu, Kristo Yesu.

Na hilo lilikuwa agano ambalo Mungu alikuwa anaandika kwalo, pale ambapo Mungu alipofanyika mwanadamu miongoni mwetu, basi yeye alichanwa vipande viwili. Unaona, hao watatu, wenye umri wa miaka mitatu, ndipo wachanwe vipande viwili viwili. Na Mungu alipeleka sehemu moja ya Hicho Nyumbani pamoja na Yeye, na kutuma ile sehemu nyingine chini hapa. Sasa ule Mwili unapokutana tena, itapasa uwe ule ule Uzima uliotawala ule Mwili utapasa uwe Uzima ule ule unaotawala huu Mwili. Na Yeye alikuwa Neno. Na Yeye ndiye Neno! Unaona? Na matendo ambayo Neno lilitenda wakati ule hufanya kitu kile kile leo hii. Yeye ni Neno, lile Neno la Milele. Na Neno la Mungu ni la Milele. Vema.

23 Sasa Yeye alikuwa anafanya nini? Akiweka njia, akionyesha, akijua kuwa Israeli, uzao wa asili, ungelimkataa Yeye; lakini akijua kuwa ule Uzao wa kifalme, siyo kutokana na jambo la tendo la jinsia na Sara, bali kutokana na imani aliyokuwa nayo Abrahamu, ile iliyomleta Kristo, huo ndio Uzao wa kifalme wa mataifa yote, uliochanganyikana, Bibiarusi akitoka kwenye mataifa yote. Abrahamu baba wa mataifa, siyo kwa sababu yeye alikuwa…aliishi na mke wake, Sara, na kumzaa mwana, bali kwa sababu yeye aliamini Neno. Amina. Hilo ndilo jambo lenyewe.

24 Sasa tunaona, baada ya huu, huu uzoefu mkuu. Sasa tunakuja kwenye sura ya 17. Tunakwenda kujaribu kufikia sura ya 22 kama ikiwezekana. Ile sura ya 17. Je, unaipenda ile safari pamoja na Abrahamu? Napenda tu kuitazama hiyo. Kwa sababu ya nini? Kila kitu yeye alichofanya kilikuwa mfano mkamilifu wa Kanisa. Je, mnaamini hilo? Angalia, Maandiko yote ni mfano wa hilo.

Mtazame Yoeli, alisema, "Itakuwa katika siku za mwisho, kwamba Mungu angelimwaga Roho Wake." Jinsi gani kwamba angelikuja parare na kulila kanisa Lake! "Kile tunutu alichosaza, yule parare; na parare, madumadu." Na ni mdudu yule yule, mdudu yule yule katika hatua nne tofauti. Kila mmoja alikula sehemu. Hapa akaja yule madumadu wa kale au parare na kula gome, na yule mwingine akala tunda, na-na ndipo wakaja pale hao wengine walionyonya uhai kutoka kwenye huo. Hapo ndipo…

25 Kristo, huo Mti uliokuwa katika Bustani ya Edeni! Kulikuweko na miti miwili katika Bustani ya Edeni. Hii miti miwili iliwekwa pale kwa ajili ya kusudi la uzao. Na wakati … Hawa, yeye alikuwa mti wa mauti kama yeye aliguswa. Na Kristo alikuwa Mti wa Uzima. Sasa kwa njia ya mwanamke mauti ikaja; kwa njia ya Mtu ukaja Uzima.

Sasa Yeye aliposimama hapa akizungumza na Wayahudi, Yeye alisema, "Mimi…zenu…"

Wao walisema, "Baba zetu walikula mana jangwani kwa miaka arobaini."

Yeye alisema, "Na wao, kila mmoja, alikufa! Lakini Mimi ndimi huo Mkate wa Uzima. Mti wa Uzima utokao kwa Mungu Mbinguni, kwamba mtu aulaye huu Mkate na kamwe hatakufa."

26 Mungu aliweka Maserafi pale, wakiulinda huo Mti, kwamba hakuna mtu angeliugusa Huo. Sasa Yeye anao Maserafi nje, wakijaribu kuwaingiza katika huo Mti. Ndipo wao-wao waliona ono, wao waliutaka huo Mti, kurejea pasipo upatanisho. Lakini sasa baada ya kufanyika upatanisho, yule Mwovu anawapofusha, akiwageuzia upande huu mbali na huo Mti. Angalia.

Kristo alipokuja duniani, Yeye alikuwa Mti mkamilifu wa Mungu. Daudi alimwona Yeye katika Zaburi ya 1, akasema, "Mti uliopandwa kandokando ya mto, mito ya maji." Mito mingi, Maji moja; karama nyingi, Roho yule yule. "Majani Yake hayatanyauka."

Lakini Yeye alipokuja duniani, kulitukia nini? Nguvu ya Kirumi iliukata huo mti na kumtundika Yeye juu ya mti uliotengenezwa na mwanadamu. Ndipo Mungu alipoufufua huo Mti na kuuweka Huo mkono wa kuume, na kumtuma Roho ili kumwandaa Bibiarusi kwa ajili Yake, kama ambavyo Adamu angekuwa naye katika Bustani ya Edeni. Na huo mti ulipoanza, ulikuwa mti wa kipentekoste.

27 Tunamsikia papa akisema, "Makanisa yote, rejeeni kwenye kanisa mama, penye mwanzo. Rejeeni Rumi!"

Natamani mwanahistoria mmoja, mhudumu mmoja, au mtu fulani asimame, anitazame usoni na anionyeshe mimi kwamba kanisa lilianzia Rumi. Kanisa lilianzia Yerusalemu penye siku ya Pentekoste! Hapo ndipo. Shirika la dini lilianzia Rumi, miaka mia tatu na kitu baadaye. Lakini Kanisa lilianzia penye Pentekoste; Mungu akiuinua mti wa ukoo wa Bibiarusi kwa ajili ya Kristo, pamoja na Roho yule yule aliyekuwa ndani ya Kristo, akiuinua mti wa ukoo wa Bibiarusi. Na kulitukia nini? Na huo ulipoanza kugumia, kukua, yule mdudu wa Kirumi aliuendea na kuanza kuuvunjavunja. Kile tunutu alichosaza, madumadu alikula, hadi akaenda moja kwa moja hadi kwenye shina.

Lakini Mungu alisema, "Nitarejesha, asema Bwana." Huo mti unakwenda kuja tena, kwa ajili ya Mti wa ukoo wa Bibiarusi unamjia Bibiarusi.

28 Luther akaja, yeye alifanya nini? Akifuata kuhesabiwa haki.

Hivyo ndivyo kabisa kanisa lilivyoingia ndani, Yohana akihubiri kuhesabiwa haki. Kristo akaingia ndani, akihubiri utakaso, Waebrania … Namaanisha Yohana Mtakatifu 17: 17, "Watakase hao kwa ile Kweli, Baba. Neno Lako ndiyo ile Kweli." Na Yeye alikuwa Neno. Hilo ni sahihi. Yeye alikuwa Dhabihu. Ndipo penye Siku ya Pentekoste, pamoja na Roho Mtakatifu. Kuhesabiwa haki; utakaso; na wakati huo mti ulipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, huo ulikuwa mti mkamilifu wa ukoo wa Bibiarusi.

Warumi waliula huo na kuumaliza. Kama tu jinsi ambavyo huo ulimalizika, huu uliinuka! Na ulipoanza kuinuka kupitia Luther, nini? Baada ya kifo cha Luther wao waliliunda hilo kuwa shirika la dini. Yule Mume alifanya nini? Alikata na kuondoa yale matawi ya mizabibu ya kale yaliyokufa.

Hilo likaenda, mbali zaidi, moyo wa mti ukikua. Ni mti uliochaguliwa tangu asili! Ile Mbegu imekaa pale, ikatokea juu! Nayo ikainuka tena, na Wesley alianza. Na walikuwa na uamsho mkuu chini ya utakaso. Kulitukia nini? Yeye aliondoa matawi tena, wao walipounda shirika la dini. Kamwe shirika la dini lilikuwa halijawahi kuinuka. Kamwe lile lililowahi kuanguka halikuwahi kurejea tena.

29 Ndipo wakaja Wapentekoste pale, walikuwa na kurejeshwa kwa karama. Hilo lilifanya nini? Liliunda shirika la dini! Mungu alifanya nini? Alilikatilia mbali.

Lakini Yeye alisema nini? "Nitarejesha, asema Bwana." Yeye ataleta kutoka kwenye huo mkusanyiko, Kanisa lililooshwa kwa Damu, lililonunuliwa kwa Biblia, na lililoimarishwa kwa Neno, Bibiarusi! Zile nuru za jioni zinatokeza. Tunda huwa linaiva wapi? Pale pale kwenye kilele cha mti. Ninapoendelea tena hapa.

Turejee kwa Abrahamu, nyuma, hebu tumwendee Abrahamu. Yeye anakuja hapa, Uzao wa kifalme ukiingia ndani wakati wa jioni. Mataifa…Angalia sasa baada ya sura ya 17, tuliona hapa katika sura ya 17, Mungu alimtokea Abrahamu katika Jina la Mungu Mwenyenzi.

30 Abrahamu alikuwa na umri wa miaka tisini na tisa, na wakati wote huu kamwe hakuyumba, bali aliliamini Neno la Mungu; na kuita yale mambo yasiyokuwepo kama kwamba yalikuwepo, kwa sababu Mungu alisema hivyo, bado akiamini yule mtoto angekuja, akishikilia ile ahadi. Ni mtu aliyoje! Ni ndugu aliyoje! "Abrahamu, ambaye dhidi ya tumaini…Tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa. Abrahamu alikuwa tasa. Mwili wa Abrahamu ulikuwa umekufa. Biblia ilisema ulikuwa umekufa, kwamba mwili wake ulikuwa kama uliokufa. Na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa. Na Sara sasa alikuwa amekaribia sana miaka arobaini tangu akome hali ya kike, na bado Abrahamu aliliamini hilo, kwamba Sara angelikuwa na yule mtoto kwa sababu Mungu alisema hivyo. Hilo ndilo jambo lenyewe. Akilishikilia Neno kwa sababu Mungu alisema hivyo! Haidhuru kitu gani, zile kanuni za imani za dini zilizolifunika Hilo, na bado hilo Neno lilikaa pale! Ilipasa hiyo ije. Na hilo Neno likiwa limekaa katika moyo wa Abrahamu!

Haidhuru ni miaka mingapi, "Siku za *hili* zimekwishakupita, na *lile* pale." Maadam hilo Neno limekaa pale, litakuwa la uumbaji, kwa sababu hilo ni Neno lililomea. Kwani, Mungu ni Neno, na Uzima wa Mungu uko katika Neno. Angalia sasa wakati lile Neno lilipodondoka ndani ya Uzima wa Mungu, kitu fulani kilitukia, hicho hutukia.

31 Sasa tazama.

Ndipo Yeye alipomtokea Abrahamu katika Jina la Mungu Mwenyenzi. Sasa, Mungu

anayo majina saba ya ukombozi yaliyounganika kufanya kuwa mmoja. Na Yeye alimtokea Abrahamu hapa katika umbo la Mungu Mwenyenzi ambalo humaanisha "El Shadai." Katika…"Shadai," katika Kiebrania. *El* humaanisha "mwenye nguvu." *Shad* humaanisha "titi," kama titi la mwanamke. Na sasa badala ya kuwa "shad," umoja; "Shadai," wingi. Sasa ni faraja tamu iliyoje kwa mwanamume mzee, mwenye umri wa miaka mia, akishikilia Neno la Mungu moyoni mwake, na kuisikia Sauti ya Mungu ikimjia na kusema, "Mimi ni El Shadai. Mimi ni Mungu mwenye Matiti."

Tunayo faraja iliyoje! Sasa, sasa, kumbuka, siyo tu "mwenye matiti," bali "mwenye matiti"! Aliyejeruhiwa kwa ajili ya maovu yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tulipona."

32 Sasa, mama hufanya nini, kwa mtoto wake mdogo, mtoto awapo mgonjwa na kutaabika? Yeye humchukua yule jamaa mdogo. Yeye humshikilia kwenye titi lake, na mama…na yeye hunyonya nguvu za mama yake na kuingiza katika mwili wake mwenyewe kupitia titi. Na siyo tu yeye anatosheka au yeye…Yeye anatulizwa. Yeye anapiga kelele kwa sauti yake ya juu, yeye anakuwa amesumbuka sana; lakini yule mama anapomnyanyua na kuweka…kumweka kwenye titi, na kuanza kumvumishia wimbo, akimtingisha nyuma na mbele kumbembeleza mtoto, yeye anamhisi mama yake, kichwa chake kinakuwa juu ya kifua cha mama, na yeye anaanza kunyonya na kuvuta nguvu kutoka kwa mama yake, kuingiza ndani ya mwili wake. Yeye anajipa tena afya mwenyewe, akijenga nguvu; na pia kutosheka, wakati siku kwa siku yeye anakua na nguvu zaidi na zaidi.

33 Ni uzoefu ulioje kwa ule Uzao wa Abrahamu! Yeye bado ni Mungu Mwenyenzi, El Shadai! [Mungu Mwenye matiti] Tunaweza kushikilia ahadi yoyote Yeye aliyoifanya katika Biblia. Uzao Wake, watoto Wake, kama wewe ni mgonjwa, shikilia tu hilo titi la ahadi ya Neno lililosema, "Kwa kupigwa Kwake tulipona." Hilo linatosheleza. Nasi tunavuta wakati wote, nguvu zetu, kutoka kwa Yule mwenye nguvu, El, Yule mwenye nguvu, Yule wa Milele, tukivuta Uzima Wake kutoka Kwake, kupitia ahadi Yake.

Hilo linampa mtu kujisikiaje kulala juu ya kifua cha El Shadai, ukiamini, tukijua kuwa tunanyonya nguvu Zake Kristo, kutoka kwenye ahadi Yake, kuingia ndani yetu!

Wakati El Shadai alipomwegemeza Abrahamu juu ya kifua Chake, miaka ishirini na tano hapo kabla; mwanamume mzee, mwenye umri wa miaka sabini na tano, na mke wake miaka sitini na tano; kamwe yeye hakuondoka kwenye hilo Titi. Yeye alitembea moja kwa moja kuvuka nchi ya kigeni, miongoni mwa wageni ambao hawakumjua Mungu, lakini yeye aliendelea kutoa ushuhuda, na alikuwa imara katika imani, akimtukuza Mungu, kwa sababu yeye alijua yeye alikuwa anavuta kutoka kwenye ile ahadi.

34 Ni tumaini lililoje kwa ajili ya kanisa jioni hii, katika saa ya giza, ushirikina, msisimko, kuzingatia zaidi usomi. Roho Mtakatifu alisema, "Katika siku za mwisho, kutakuja kanisa lenye kuzingatia zaidi usomi. Roho, anena waziwazi," Timotheo wa Kwanza 3, "katika nyakati za mwisho baadhi watajitenga na Imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mapepo," hakika, "wenye mfano wa utauwa." Wao walikuwa wanafanya nini? "Wenye kiburi, wenye majivuno." Daktari, Ph.D., LL.D., QST, vyeo vyote hivi. "Mbona, Daktari *Fulani*, wakati *fulani*, ni mchungaji wetu."

Ni bora mtu fulani, akiwa familia yangu au mtoto wangu, ambaye hajui tofauti kati ya maharage yaliyomenywa na kahawa, na kumjua Kristo. Hilo ni sahihi. Unampeleka nje kule mahali fulani kando penye kisiki na kupiga magoti kwa magoti yake na kuomba pamoja naye hadi Roho Mtakatifu aje Kwake. Ni bora niwe na huyo kuliko saikolojia ambayo ungeweza kuimwaga ndani yake kwa njia ya shahada ya daktari. Mwambie Neno la Mungu! Ndiyo.

35 "Lakini wenye kiburi, wenye majivuno, wapendao anasa zaidi kuliko wampendao Mungu, wavunjao maagano, wasingiziaji, wasiojizuia, na wanaowadharau hao walio sahihi."

Ee, unasema, "Hao ni wakomunisti." Hapana, hapana! Hao ni wanaoitwa Wakristo.

"Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu Zake, hao nao ujiepushe nao. Kwa maana katika hao wamo wale wanaokwenda nyumba hadi nyumba, wakiwaongoza wanawake wajinga, waliochukuliwa na tamaa nyingi, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli." Hilo ni sahihi. Hilo ndilo jambo lenyewe. Na tunaiona ile siku.

36 Na ni faraja iliyoje kwa mwamini, kujitenga mwenyewe mbali na kutokuamini kote,

kanuni zao zote za imani za dini zilizo kinyume cha Mungu, mafundisho yao yote yaliyo maovu, na utazame moja kwa moja kwa Kristo na ulichukue Neno, na ulishikilie hilo Neno hadi ulione Hilo likidhihirishwa. Haidhuru utasubiri kwa muda mrefu jinsi gani, dumu pale! Mungu aliahidi hilo. Yeye alikuongoza kwenye hilo, lishikilie hilo. Dumu pale. Usirudi nyuma. Dumu pale pale! Kama una hakika na hilo, utadumu pale. Lakini kama unayumba, usilegee penye kitu chochote kidogo. Kima huparamia vitu vyovyote vinavyong'ara, lakini dubu hushikilia kile alichokishikilia. Hivyo, dumu moja kwa moja! Ndiyo, endelea kushikilia, kushikilia vizuri!

37 El Shadai! Yeye alisema, "Mimi ni El Shadai. Abrahamu, Mimi ni Mwenye nguvu. Wewe ni mzee. Wewe una umri wa miaka mia. Sasa, nguvu zako zimekwisha; lakini Mimi ndiyo Nguvu zako! Tumaini lako lote limeondoka; lakini Mimi ni Tumaini lako!

Ee, ukiteseka, jioni hii, na nje hapa ukiwa na saratani na vitu, je, huwezi kuona Nguvu zako zinatoka wapi? Siyo kutoka kwenye kisu cha daktari mpasuaji, bali kutoka kwenye Neno la Mungu! "Mimi ni Sehemu yako! Mimi ni Nguvu zako! Unavuta nguvu zako kutoka Kwangu!"

Siyo kumpuuza daktari mpasuaji sasa; yeye hufanya sehemu yake ambayo ni juu yake. Lakini Mungu ndiye Mponyaji. Hakuna daktari mpasuaji, hakuna daktari, hakuna dawa iliyowahi kuponya. Hapana, bwana, wao hawana dawa hata moja itakayoponya. Sasa, daktari yeyote atakuambia hilo! Wao wanayo misaada, lakini Mungu ndiye Mponyaji. Wao wanaweza kukata mshipa katika mkono wako, lakini inampasa Mungu auponyeshe huo. Wao hawana chochote cha kujenga misuli ya mwili; kama wangeweza, wao wangemtengeneza mtu. Hivyo mnaona, Mungu ndiye Mponyaji. Unaweza kurekebisha mfupa, lakini Mungu inampasa auponye huo. Mungu ndiye Mponyaji, "Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote." Na huwezi kufanya Neno la Mungu liseme uongo; litarejea moja kwa moja kwenye ukweli kila wakati, litarejea tu moja kwa moja. Huwezi kulifanya Hilo liseme uongo.

38 Sasa wao husema Biblia inajipinga Yenyewe. Nimeuliza, na kuwaambia watu ningewapa mishahara ya mwaka shambani, kama mimi ningeweza, kila kitu ambacho nitaweza, wanionyeshe Neno moja katika Biblia linalopingana na lingine. Hilo ni sahihi. Hilo halipatikani. Ni kwa sababu akili zako za kimwili zinalitazama hilo jinsi zinavyofanya. Roho Mtakatifu ni Mfasiri wa hilo Neno. Hilo Neno ni kweli, limewekwa pamoja. Lote liko pale kama mafumbo ya kulinganisha mambo, lakini linamhitaji Roho Mtakatifu kuliweka hilo pamoja, ili kulifanya Hilo picha ya Mungu ya ukombozi na baraka Zake kwa watu Wake. Amina. Halijipingi Lenyewe! Hakuna Andiko moja, wala aya moja ya Hilo, inayoipinga nyingine. Kama ni hivyo, hilo halistahili hiyo karatasi lililoandikwa juu yake, hilo linadanganya. Mungu hadanganyi. Mungu ni mkweli, mwenye haki, mtakatifu, mwaminifu. Yeye ni Mungu.

39 Sasa, Abrahamu alipopata hili neno, kuwa, "Mimi ni El Shadai. Mimi ni Mpaji-Nguvu wako! Mke wako, tumbo lake la uzazi limekwishakauka, yeye amekwishakupita hali yake ya kike kwa miaka arobaini, mwili wako ni kama uliokufa; lakini Mimi ni El Shadai." Yeye alimleta tu Ishmaeli, un anajua; lakini Yeye alisema, "Siyo huyo. Hapana, yeye atakuwa mtu mkuu. Yeye anakwenda kuwazaa wafalme wengi mno. Lakini yule niliyefanya ahadi, ni kati yako na Sara." Hilo ndilo jambo lenyewe! Amina. Abrahamu alijisikia vizuri hasa.

Yeye alisema, "Sasa nataka nikuambie jambo fulani, Abrahamu. Mimi nakwenda kubadili jina lako." Yeye alisema, "Wewe hutaitwa tena *Abramu*, bali Abrahamu." *Abramu* humaanisha "baba wa juu-juu." Lakini Abrahamu humaanisha "baba wa mataifa." Na siyo S-a-r-a-i tena; yeye ni S-a-r-a, *Sara*, "malkia." Alibadili jina lenu! Ni jina lililobadilishwa iliyoje! Jambo fulani lilitukia kwa sababu wana…Unaona, inapasa pawepo na badiliko kabla mambo hayajatukia. Yeye hakuweza kuwapa mtoto maadam majina yao yalibakia hivyo.

40 Nawe huwezi kuzaliwa mara ya pili maadam jina lako linabakia nje ya Kitabu cha Mbinguni. Unaweza kuliweka hilo kwenye kila kanisa, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, ukilichukua kutoka mahali hadi mahali, ukihangaika na wote; lakini inapasa hilo liwekwe kwenye Kitabu cha Mbinguni kabla kitu chochote hakijaweza kutukia, na uumbaji mpya unaweza kuja. Kabla uzima mpya haujaja, majina yao inapasa yabadilishwe. Mwaweza kubadili yenu, pia, kutoka kwenye baadhi ya hivi vitabu vilivyotengenezwa na mwanadamu, kwenda kwenye Vitabu vya Mbinguni.

"Na pale, jina lako siyo tena *Abramu*, 'baba wa juu', bali ni *Abrahamu*, 'baba wa

mataifa.' Siyo (Sara) *Sarai* tena, Sarai; bali Sara, 'malkia!"

41 Ee, sasa tunakuja hapa kwenye sura ya 18. Kutoka sura ya 17, hebu twendeni moja kwa moja kwenye ya 18, kwa sababu tu ni…Sitaki kwenda mbali zaidi na hilo jioni hii, kuwaweka hapa, kwa sababu nataka mrudi kesho jioni. Sasa tazameni. Na tutafikia, kwa haraka tu tuwezavyo, kwenye ile ya 22. Tazameni sasa. Ilipofikia kama siku moja, labda, tuseme, siku mbili au tatu baada ya hilo, Abrahamu na Sara, mahema yao yaliwekwa.

Kule chini mjini chini kule, namwazia Bibi Lutu alikuwa amevaa magauni yote ya mtindo mpya, waliyokuwa nayo chini kule. Na alikuwa anatengeneza nywele mitindo yote kote na kila kitu walichokuwa nacho. Yeye alikuwa anaishi tu kianasa, na mabinti zake walikuwa vivyo hivyo. Vivyo hivyo tu yule mama kahaba wa kale alivyofanya leo hii, na kufanya mabinti zake wote wafanye kitu kile kile.

Sasa, lakini Sara, bado akiwa mwanamke mzuri wa sura kuliko wote katika nchi yote, alikaa katika nchi kame, kwa sababu alikuwa anamshikilia yeye ambaye alikuwa na ile ahadi. Sasa ni vema niondoke moja kwa moja hapa, kwa sababu nitakwenda, nitakuwa … Nitawaweka ninyi hapa hadi usiku wa manane. Hilo ni sahihi. Abrahamu alikuwa na ile ahadi.

Mshikilie Kristo, Yeye Ndiye aliye na ahadi! Yeye ndiye Ahadi. Yeye ndiye Ahadi. Tazama.

42 Siku moja jua lilichomoza likiwa na joto hasa asubuhi moja, Abrahamu alikuwa ameketi kivulini mwa hema lake pale kando ya mwaloni. Na yeye akatazama chini, ni lazima ilikuwa penye saa tano asubuhi, na yeye aliwaona watu watatu wakija, wakija juu, nguo zao zikiwa na vumbi. Na Abrahamu akakimbilia nje. Kulikuweko na kitu fulani moyoni mwake kilichomfanya ajisikie vizuri hasa, na yeye akakimbilia nje na kuanguka miguuni pao. Na tazama, yeye alisema, "Bwana wangu!" Je, hilo si la ajabu? Watu watatu; lakini, "Bwana wangu"!

Mtazame Lutu. Wakati hao wawili walipokwenda chini kule, hao wawili tu, yeye alisema, "Mabwana zangu." Lutu aliwaita wao "mabwana." Abrahamu…Lutu aliwaita, wawili, "mabwana." Na Abrahamu aliwaita hao watatu, "Bwana! Bwana wangu!" Amina! Ee, wakati umekaribia! Tazama, yeye alisema, "Bwana wangu, kama nikipata neema mbele Zako, uje, uketi chini ya mwaloni. Hebu mimi nilete maji kidogo na nioshe miguu Yako, na ule kiasi kidogo cha mkate. Kwani hii ndiyo sababu pekee ya Wewe kuja hapa, ili kuniona mimi." Wao wakatembea kule.

43 Abrahamu alitoka nje na kwenda nyuma ya hema, na kusema, "Sara, kakande donge utengeneze kwa haraka, na utengeneze keki juu ya jiko." Akatoka nje na kumkamata ndama mdogo, na kumchinja na kuandaliwa, na kutengeneza vipande vya nyama, na kuleta siagi na maziwa, na-na kuviweka chini mbele za yule Mtu, nao wakala.

Na Mmoja wao alikuwa Mungu Mwenyewe! Hilo ndilo Biblia ililosema. Sasa kama unataka kubishana na Hilo, endelea. Abrahamu alimwita Yeye 'Elohimu, Mungu." Abrahamu alipaswa kujua; yeye alikuwa anazungumza na Yeye. Tazama, "Bwana Mungu!" Sasa, Mmoja wao alikuwa Mungu. Na Abrahamu alimtazama Yeye. Abrahamu akalitambua hilo. Sasa tazama pale.

44 Mhudumu fulani aliniambia wakati mmoja, yeye alisema, "Ndugu Branham, wewe humaanishi kuniambia kuwa wewe unaamini hilo, kuwa huyo Mtu alikuwa Mungu?" Mimi nikasema, "Abrahamu alisema Yeye alikuwa Mungu. Wafasiri wote wamefasiri hilo namna hiyo hiyo, herufi kubwa B-w-a-n-a. Na mtu yeyote anayesoma Biblia anajua hiyo herufi kubwa B-w-a-n-a ni Elohimu. Hutoka kwenye neno lile lile, Elohimu! 'Hapo mwanzo, Mungu aliumba,' Elohimu, Mwenyenzi, aishiye kwa Yeye Mwenyewe, 'aliumba Mbingu na nchi.' Huyo hapo tena, akiwa amesimama pale mbele yake."

Yeye akasema, "Vema, unajua," kasema, "huyo-huyo alikuwa mtu tu!"

Mimi nikasema, "Hakika, Yeye alikula nyama, Yeye alikula, akanywa maziwa, na Yeye-na Yeye alikula mkate." Nikasema, "Hakika, Yeye alikuwa Mungu."

Yeye akasema, "Hilo linawezekanaje?"

Nikasema, "Bwana, wewe-wewe…"

Mimi natumaini hayo hayaumizi hisia zenu; wao walikuwa Mashahidi wa Yehova. Na yeye akaniambia, "Vema, Bw. Branham, tazama hapa, nataka kukuambia jambo fulani.

Mungu hakuweza kufanya hilo."

Nikasema, "Wewe humjui tu Mungu wangu. Na hivyo tu." Nikasema, "Mwili wa mwanadamu umeumbwa kwa kitu gani? Petroliamu, potashi, na nuru ya ulimwnegu, viasili kumi na sita. Kitu pekee Mungu alichopaswa kufanya ili kushuka chini na kupeleleza Sodoma, Yeye alisema … alifika pale na kuchukua konzi ya nuru ya ulimwengu na petroliamu, na 'Loo!' Akasema, 'Njoo hapa, Gabrieli, ingia hapa.' Hilo ni sahihi. Akaenda pale na kuchukua konzi nyingine ya vumbi, 'Njoo hapa, Mikaeli, ingia ndani hapa." Na kutengeneza moja kwa ajili Yake Mwenyewe." Ilimpasa Yeye awakilishe jambo fulani alilokuwa anakwenda kuwa katika siku za mwisho, hivyo Yeye anashuka moja kwa moja chini na kuzungumza katika mwili wa kibinadamu. Sahihi kabisa. Ee, ninafurahi sana kwamba Yeye ni wa aina hiyo!

45 Siku fulani huenda pasiwepo na chochote kilichobakia kwangu. Mimi nimeumbwa kwa hivyo viasili kumi na sita, pia. Nilikuwa nikichana zile nywele mbili au tatu nilizobaki nazo, siku ile nyingine. Mke wangu akanitazama, na yeye akasema, "Billy, unapata upaa."

Nikasema, "Mpenzi, sijapoteza hata mmoja wa hizo."

Yeye akasema, "Ulikuwa na nywele zenye mawimbi."

Nikasema, "Naam, lakini sijapoteza mmoja wa hizo."

Yeye akasema, "Naomba uniambie ziko wapi."

Nikasema, "Basi, mpenzi, uniambie hizo zilitokea wapi kabla sijazipata. Na kokote zilikokuwa kabla sijazipata, ziko pale zikinisubiri niziendee."

Amina! Utukufu! Biblia ilisema, "Hakuna unywele mmoja wa kichwa chako utakaopotea!" Haleluya! Hilo ni sahihi kabisa. Hilo halikuweko, na bado liko; na bado haliko, basi liko. Hakika. Kabisa! Petroliamu, nuru ya ulimwengu, kalsiamu, potashi, kadhalika. Mungu…Wakati mimi ninapokuwa si chochote, hakuna chochote unachoweza kuona, majivu tu, Yeye atanena, haleluya, akitupa ile potashi na petroliamu pamoja, nami nitaishi tena katika Uwepo Wake. Haleluya! Yeye anatupa Uzima wa Milele. Amina. "Wote Baba alionipa Mimi, hakuna chochote kilichopotea, nami nitamfufua tena penye siku za mwisho." Mimi naamini hilo! Kama Uzao wa Abrahamu, naitazamia ile siku! Nautafuta Mji Ambao Mjenzi na Mtengenezaji ni Mungu. Amina. Hakika. Haidhuru huu unapata makunyanzi na kusinyaa iliyoje, na nywele kunyonyoka, haidhuru kunatokea nini, Mungu ataufufua huo tena, katika fahari ya ujana tena, penye siku ya mwisho. Yeye aliahidi tungelifanya hilo, nami nautazamia huo Mji! Amina.

46 Loo, jamani! Najisikia wa kidini mno sasa hivi, nikijua, na hilo tumaini la baraka likiwa linanisubiri Pale. Nautazamia huo Mji. Moyo wangu unagongagonga kuelekea kwenye Huo. Ee, sitageukia njia moja, bali nitatazama mbele moja kwa moja kuelekea Mahali pale. Mungu, nisaidie nidumu pale pale, mkweli na mwaminifu, nikirusha mstari wa mwisho wa uzima, kila mahali, na nikimleta kila msafiri aliyechoka niwezaye, ili kwenda pale.

Ndiyo, nilikuwa na ono la hilo siyo muda mrefu uliopita, na kuliona hilo, na kuwaona wapendwa wangu pale, wakiwa wamerejea kwenye ujana tena. Uko pale. Uko pale. Mimi najua iko pale! Ndiyo, bwana! Sasa, huenda ulisoma hilo katika jarida La Sauti la Wanaume Wakristo Wafanyabiashara, na magazeti mengi na vitu vilivyoandikwa hilo. Marafiki, hilo halikuwa ono. Nimeona maono, najua, napaswa kujua yana nini, kwa makumi elfu Yeye aliyonipa mimi. Lakini hili halikuwa ono. Nilikuwa pale, nikiwa nimesimama pale pale, nikitazama nyuma. Na najua wewe uko pale. Uko pale, marafiki, mko pale! Mimi najua mko pale! Ndiyo! Kama tu kwa hakika kama nilivyosimama hapa, hivyo nisaidie, kama ninazo akili zangu timamu na nikiwa nimesimama hapa katika haya madhabahu, huo uko pale! Mungu ameweka ahadi Yake, na hiyo ni kweli, ni kweli mno! Ndiyo, bwana. Huo uko pale.

47 Tazama.

Sasa tunaona, huyu Mtu aliketi chini na kula. Na wawili kati yao walisimama na kwenda chini Sodoma. Mmoja alikaa na Abrahamu. Hebu tutazame mazungumzo yao. Waliendelea kutazama kuelekea Sodoma. Na Abrahamu alijua kulikuweko na kitu fulani cha kigeni kidogo juu ya huo. Hivyo Yeye akasema, basi Yeye alipokuwa tayari kuondoka, Yeye alisema, "Unafikiri nitamficha Abrahamu; yeye akiwa anakwenda kuwa

baba wa mataifa, najua jinsi yeye atakavyowalea watoto wake, na kadhalika; hicho kitu ninachokwenda kufanya?" Yeye akasema, "Dhambi za Sodoma zimehuzunisha mno hadi imeingia masikioni Mwake." Yeye ameshuka chini kuchunguza.

48 Sasa kumbukeni, kama nilivyosema usiku ule mwingine, wawili kati ya hao wajumbe walikwenda chini katika Sodoma, nao waliwahubiria hao Wasodoma; na waliwapofusha hao usiku ule, kwenye Neno. Lakini, kumbukeni, kulikuweko na Mmoja; wao, walikuwa na ishara yao, Mgeni miongoni mwao.

Mtazame Lutu. Lutu ameketi penye lango, na kusema, "Mabwana zangu." Na kuishi namna hii! Wao walisema, "Ingieni nyumbani mwangu." Yeye alisema, "Sisi tutalala barabarani." Ni nyumba iliyoje!

Lakini mara tu Abrahamu; wao walisema, "Hili ndilo kusudi tulilojia. Tutaketi chini hapa kando yako."

49 Hiyo ndiyo njia. Ishi hivyo, kwamba kama Mungu angelitaka kukutumia, Yeye anajua pale pale pa Yeye kuja ili kukupata. Wewe uko katika nafasi, ukiishi ukiwa maisha safi mbele za Mungu, maneno yako ni ya ukweli. Hapo ndipo aina ya mahali ambapo Malaika huja. Mtazame Elizabethi na Zakaria, unaona, msimamo mwadilifu, wakitembea katika Amri zote za Bwana. Hivyo ndivyo tunavyotaka kuishi, hivyo Mungu anapokuwa tayari kukutumia, Yeye anasema, "Hawa ni watu Wangu. Naweza kufanya kile ninachotaka na hili kanisa. Wao wananiamini Mimi. Wao wanasimama juu ya Neno Langu." Unaona. Hivyo ndivyo unavyotaka kufanya, ishi hayo maisha.

50 Sasa tunakuta huyu Malaika, Yeye alisema, "Sitamficha Abrahamu. Lakini nitakutembelea kulingana na wakati wa furaha mno." Na tazama, Yeye hakumwita Abram, Yeye alimwita "Abrahamu." Mungu alijuaje kuwa hilo jina lilikuwa limebadilishwa? Yeye alikuwa Ndiye aliyebadili hilo. Hakika. Tazama, kamwe hakumwita Sarai, unajua, S-a-r-a-i, S-a-ra, "Mkeo yuko wapi, Sara?" Mungu alijuaje kuwa yeye alikuwa ameolewa? Yeye alijuaje Abrahamu alikuwa na mke, na jina lake lilikuwa Sara?

Na Abrahamu alisema, "Yeye yuko katika hema nyuma yako."

51 Ni bibiye aliyoje!

Leo, wanawake ni wenye makelele mno! Kila…Mume wao hata hawezi kuongea. Inawapasa wajitokeze moja kwa moja nje pale, sigara mkononi mwao, wakiwa wamevaa kaptula, wakiwa ndio pekee wanaozungumza. Ni jamii ya watu iliyopotoka iliyoje, inampasa mwanamke awe mpishi mkuu na mwoshaji wa chupa, kila kitu kingine! Yeye anapoondoka jikoni, yeye anaondoka sehemu yake ya wajibu, sawa, kama mama.

Sasa tunakuta, wanawake wakati ule walibaki nyuma na kujiheshimu, walitenda kama akina bibiye, kiongozi wao ndiye aliyefanya maamuzi na mambo.

Na unajaribu kumwacha mwanamume fulani amwambie mke wake; mke anasema, "Nitakufanya uelewe sasa hivi!" [Ndugu Branham anapuliza-Mh.] akipuliza huo moshi kutoka kinywani mwake, akionekana hivi, ni muonekano wa kuchukiza ulioje. Kamwe sikuwahi kuona kama huu! Na unaweza kuwazia nje kule, na usimame pale ukimtazama yule mtu, ukitambua ile roho ndani pale, na hivyo vitu; na huenda akiimba katika kwaya katika kanisa fulani. Ee, siku kama hii tunayoishi! Si ajabu tuko penye ile siku! Mimi-mimi natumaini mnaweza kudaka kupitia mistari kile ninachomaanisha.

52 Tazama, hilo lilikuwa pale. Sara alikuwa ndani ya hema, yeye alikaa ndani mle na kujiheshimu. Abrahamu alikuwa anafanya makaribisho ya hawa Malaika. Sasa, na Yeye alisema, "Nitakutembelea."

Na Sara alikuwa anasikiliza. Na yeye alicheka kimoyomoyo, akasema, "Mimi, mwanamke mzee, nikiwa mzee kama nilivyo, na pale bwana wangu mzee pia, na aseme kuwa tunakwenda kuwa na furaha tena kama mume na mke?" Na yeye akacheka.

Na yule Malaika, akiwa amepiga kisogo, alisema, "Mbona Sara amecheka?"

Kumbukeni, hiyo ilikuwa ishara ya mwisho ambayo ule Uzao wa…au Abrahamu mwenyewe, ambao ni mfano wa Kanisa, hiyo ilikuwa ishara ya mwisho ambayo yeye aliipokea. Katika ishara zote zile nyingine ambazo yeye alizipokea, hiyo ilikuwa ya mwisho kabla Sodoma haijaangamizwa. Je, hilo ni sahihi? Ile ishara ya mwisho!

53 Wakati Israeli, ule uzao uliomfuata Abrahamu. Na Wasamaria, ambao walikuwa uzao uliotupwa wa mbegu iliyochanganyikana, wakiwa wanamtafuta Yeye, hata hivyo;

wao walisema, "Baba yetu-yetu Yakobo alitupa hiki kisima," yule mwanamke alisema pale Sychar, Unaona? "Baba yetu Yakobo, yeye-yeye alimpa Yusufu hiki kisima, mwanawe, na-na tumekuwa tukinywa kwenye hicho, na yeye aliwapa maji ngamia wake. Na Wewe unasema unayo maji kiasi, na kadhalika namna hiyo?" Unaona? Na ile ishara ya mwisho ambayo uzao wa Israeli, kimwili, walipokea, ilikuwa aina ile ile ya ishara! Loo! Je, huwezi kuona hilo? Waza kwa dakika moja!

Ile ishara ya mwisho ambayo Abrahamu pamoja na agano, ile ishara ya mwisho kabla ya kukataliwa kwa kanisa vuguvugu, na maangamizi yake, ilikuwa ni ishara ya kutambua mawazo ndani ya mioyo na akili, Mungu alidhihirishwa katika mwili.

Na ishara ya mwisho ambayo Israeli waliona kabla wao hawajakatiliwa mbali, ilikuwa kitu kile kile. Nao walisema, "Ni Beelzebuli, mpiga ramli."

54 Sasa ndio ile saa! Mungu, hebu hili lizame ndani! Sasa ndio ile saa, ambayo, ule Uzao wa kifalme wa Abrahamu! Je, mnalielewa hilo? Mungu alidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, aliwapa ishara yao ya mwisho kabla ya maangamizi ya lile lililo vuguvugu na kuondoka kama lilivyofanya. Mwisho! Ufahari wa mwisho wa kurudi nyuma kwa Lutu! Hebu hilo lizame kwa dakika moja tu.

Abrahamu, moja; uzao wa kiasili wa Abrahamu, mbili; Uzao wa kifalme wa Abrahamu, tatu.

Tazama, Ujumbe hauchukui walio vuguvugu nje kule. Wapi hata ulikowaendea hao? Ulitumwa kwa wapentekoste, wateule, waliovutwa nje.

Na kama ambavyo Israeli walifanya wakati ule, tisini … Tazama ni wangapi, tazama ni Israeli wangapi walioupokea Huo. Wakati ulipowadia kwa ajili yao ili kwenda juu kule, kulikuweko na mia na ishirini kati ya kama milioni nne.

55 Sasa tazama ule Uzao wa kifalme. Unaona, inapasa uje hizo nyakati tatu, unaona, kila mahali unapochukua. Watu wa Hamu, Shemu na Yafeti. Ule Uzao wa kifalme wa Abrahamu! Kuna Abrahamu; ule uzao wa asili; ule Uzao wa kifalme. Kila kitu! Ule Uzao wa Kifalme ni kwa njia ya Kristo, kupitia…Tunakuja kwenye ahadi ya Abrahamu ile ambayo Mungu alimpa kupitia Kristo, ule Uzao wa kifalme. Na huu ndio Uzao wa kifalme, hili Kanisa la Bwana Yesu ambalo Yeye analirejesha katika siku za mwisho. Ule Uzao wa kifalme! Tazama, yeye aliipokea hiyo ishara! Na ule Uzao wa Kifalme Yeye Mwenyewe alisema, Yeye alipokuwa hapa, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana adamu." Huo Uzao wa kifalme, Uzao wa Abrahamu, walioitwa nje; Lutu pia, wa ndugu yake, vuguvugu, chini katika Sodoma; na ndipo Wasodoma, ulimwengu. Leo hii, ulimwengu; kanisa na ulimwengu na huo Uzao wa kifalme. Kabisa, wao wamejipanga kwenye nafasi zao za kila kitu, kabisa tu kulingana na utaratibu. Na Mungu, pamoja na ahadi Yake ameshuka chini moja kwa moja, akidhihirisha kitu kile kile. Amina. Kama hilo siyo kamilifu, mimi sijui ukamilifu ni nini. Hilo ni Andiko!

56 Mlikuwa na kunena kwa lugha, kucheza katika Roho. Mmekuwa na hii misisimko yote, na mmeona miujiza ya uponyaji, na-na viti vyenye magurudumu, na kadhalika. Tumeona yote hayo. Lakini hapa, hapa kuna ishara ya mwisho iliyokwishakuja sasa. Abrahamu aliona aina zote za mambo Mungu aliyofanya kwa ajili yake njiani, hakika, lakini hapa inakuja ishara ya mwisho, kabla ya kuja kwa mwana wa ahadi. Na sasa huo Uzao wa kifalme unamtazamia Mwana wa ahadi. Haleluya! Je, sisi, je, sisi tunamtazamia Mwana wa ahadi? Kurudi kwa Mwana wa Mungu! Haleluya! Ee, hilo linanifanya mimi nijisikie kama kupiga kelele. Tazama. Huo Uzao wa kifalme unamtazamia Mwana wa ahadi. Kama ambavyo Abrahamu alifanya chini kwa miaka kadha, akitazama, akilishikilia Neno, ndivyo kwa huo Uzao wa kifalme. Na huo Uzao unatazamia kuja kwa Mwana huyu, kuja kwa Bwana, kupitia lindo la kwanza, lindo la pili, lindo la tatu, na kuendelea hadi lindo la saba, na hapa bado tunautazamia huo Uzao wa kifalme. Na tunaona nini kabla tu ya Kuja kwa Bwana? Nini kinatukia? Mungu anashuka chini miongoni mwetu akionyesha huo Uzao wa kifalme kama Yeye alivyofanya uzao wa Abrahamu; na Abrahamu, na uzao wa Abrahamu, na huu hapa pamoja na Uzao wa kifalme. Mungu akikaa mingoni mwetu katika umbo la Roho Mtakatifu, akitenda mambo yale yale Yeye aliyotenda nyuma kule, akitenda, akionyesha kuwa ni lile lile.

57 Na kwenye utafiti wa kisayansi juu ya hiyo picha, ulimwengu unajua, ulimwengu wa kisayansi unajua hilo ni kweli.

Kanisa linajua kuwa hilo ni kweli, ulimwenguni kote.

Nami naamini kila Uzao uliochaguliwa tangu asili ndio tu kama umekwisha ingia ndani, mlango kama karibu kufungwa, na hukumu inajiandaa kugonga. Hilo ni sahihi. Mungu hatashindana siku zote na mwanadamu. Yeye atafanya kila kitu Yeye awezacho. Lakini ile saa inakaribia, marafiki. Tazama.

Nitawapa kitu fulani ili kuwasaidia sasa. Kumbukeni, ni kitu gani kilichofuata kutokea sasa? Kabla wao kuweza kupokea uzao wa kifalme, ilipasa pawepo na kutukia kwa muujiza kwa wote wawili Abrahamu na Sara, kimwili, kabla hapajakuweko na uzao wa kifalme … au kabla yule mzao hajazaliwa. "Sasa, mwili wa Abrahamu ulikuwa kama uliokufa," Biblia inasema hilo. Sivyo? "Na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa," Biblia ilisema hivyo. Sasa ilipasa pawepo kitu fulani cha kimwili kilichotukia kabla yule mzao kuweza kutokea, mwana wa ahadi. Kabla yule mwana wa ahadi kutokea, ilipasa pawepo na kitu fulani cha kimwili kilichotokea katika mwili wao, kabla ya kutokea kwa mwana wa ahadi. Tazama kile Yeye alichofanya. Nitawapa kitu fulani kidogo.

58 Sasa, kusoma Biblia. Ni Habari ya upendo kwa Mungu aliyoandikia Kanisa Lake. Ni Mungu. Mungu ni upendo. Je, mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Na Biblia imeandikwa ili kwamba wenye elimu na werevu wasiweze kamwe kuielewa Hiyo. Inakupasa uwe na upendo kwa Mungu ili uielewe Hiyo. Inakupasa uwe na Mungu ndani Yako. Yeye anajifasiri Mwenyewe kwako.

Sasa, ni kama tu nilivyo na mke. Ee, jinsi ninavyompenda! Nampenda kwa moyo wangu wote. Na nitakuwa nchi za ng'ambo mahali fulani na yeye ata … baada ya kupeleka watoto kulala, yeye angeniandikia barua, na kusema, "Mpenzi Billy, nimeketi hapa jioni hii, ninakuwazia. Ninaandika." Unaona, najua ni nini anachokiandika kwenye karatasi. Lakini namfahamu yeye na nampenda mno hadi kujua tu asili yake, najua yeye anamaanisha nini, hivyo naweza kusoma katikati ya misitari. Unaona?

Na Mungu anataka Kanisa Lake lisome katikati ya misitari. Siyo kusoma chochote kutoka kwenye Hilo sasa! Inakupasa kusoma katikati ya mistari ili kuona Hilo linamaanisha nini. Sasa tazama na uone, angalia kama Hilo halifanyi hivyo.

Sasa, kile Mungu alichofanya kwa Abrahamu na Sara, Yeye anawaonyesha, mfano wa Kanisa. Yeye alifanya kwao, Yeye aliwageuza wote wawili kuwa mwanamume na mwanamke vijana. Hakika, Yeye alifanya, akawarejesha kuwa vijana tena, kama tu Yeye anavyokwenda kufanya kwa kila Mzao wa Abrahamu. Haidhuru wewe ni mzee na umedhoofu iliyoje, kuna siku inayokuja wakati utakuwa kijana na mzuri tena, hilo ni sahihi, ufahari wa maisha.

59 Nilimwuliza daktari fulani siyo muda mrefu uliopita, "Niambie, bwana. Kila wakati ninapokula, ninaumba upya uhai wangu."

Yeye akasema, "Ndiyo, bwana. Hilo ni sahihi."

Nikasema, "Sasa, Mungu alisema kuwa sisi 'tulifanywa kutokana na vumbi la nchi."

Yeye akasema, "Hilo ni sahihi. Hizo mbogamboga na nyama na vitu unavyokula ni vumbi. Pale unapopata potashi na kalsiamu na vitu katika vitamini zako, basi unakileta hicho moja kwa moja kutoka ardhini. Nawe unafanywa kutokana na vumbi la nchi."

Nikasema, "Loo. Sasa, Mungu aliumba nchi kwanza namna hiyo."

Yeye akasema, "Mimi sijui lolote juu ya hilo, lakini" akasema "mimi najua kuwa sasa utakula chakula na kinajenga mwili wako."

Nikasema, "Nakuuliza wewe." Nikasema, "Basi wewe unaniuliza mimi juu ya uzao wa bikira?"

Yeye akasema, "Ndiyo, bwana. Nakuuliza."

Nikasema, "Ningependa kukuuliza jambo fulani daktari. Nieleze hili."

Yeye akasema, "Vema, kitu chochote ambacho hakiwezi kuthibitishwa kisayansi siyo kweli.

Nikasema, "Mimi nitachukua upande ule wa kinyume, kuwa kitu chochote kinachothibitishwa kisayansi hakiko hivyo, hakuna kitu chochote kwenye hicho." Na nikasema, "Vitu pekee vilivyo halisi vilivyoko katika maisha ni vitu ambavyo haviwezi kuthibitishwa kisayansi: upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, subira, imani. Nithibitishie hilo kisayansi? Na bado ni uhalisi! Mungu, Roho Mtakatifu, Malaika!" Amina!

"Imani hufanya hayo mambo. Kila kitu unachokiona kinatoka ardhini, kinatoka kwa mama ardhi, kinarejea kwa njia ile ile."

60 Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani. Mimi nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, nilikula chakula kile kile ninachokula sasa hivi. Nilikula maharagwe, viazi, na mkate, na nyama. Na kila wakati nilipokula, nilikuwa mkubwa zaidi na mwenye nguvu zaidi."

Yeye akasema, "Hakika, ulikuwa unafanywa upya uzima wako."

Nikasema, "Ni kwa nini, baada ya kupita kama umri wa miaka ishirini na mbili, mtu yeyote mwingine, haidhuru unakula kiasi gani, unakuwa mdhaifu zaidi na kuzeeka zaidi? Wazia hilo." Nikasema, "Ninalo dumu la maji hapa, na nina bilauri; na nilianza kumimina maji kutoka kwenye hili dumu lenye maji mengi katika hii bilauri, na inaanza kujaa hadi inafikia katikati; na ndipo pasipo kitu chochote chini hapa kabisa, ninapozidi kumimina ndani, yanazidi kwenda chini zaidi. Haidhuru ninakula kiasi gani, vizuri iliyoje; nakula vizuri zaidi sasa kuliko nilivyokuwa nikila, vizuri zaidi mara mia."

Najua ilikuwa ni kitu gani kutafuna ngozi za nyama usiku kucha, na kula mkate wa mahindi kwa kifungua kinywa pamoja na uji wa mtama, na kitu hicho hicho kwa mlo wa jioni na chakula cha usiku, pia. Najua ilikuwa ni kitu gani ili kujitahidi katika kuishi katika maisha, na sasa naweza kula vizuri zaidi. Namshukuru Bwana. Lakini haidhuru ninakula kiasi gani, bado nakuwa mdhaifu zaidi na kuzeeka zaidi. Na hatimaye nitakauka na kufa. Kwa nini? Kwa nini? Ni miadi aliyoifanya Mungu. Hilo ni sahihi. Ndiyo, bwana.

61 Na watazame Abrahamu na Sara, wao walirejea kwenye kama umri wa miaka ishirini na mbili au ishirini na tano.

Ee, unasema, "Upuuzi, Ndugu Branham!" Vema, sasa keti kimya kwa dakika moja tu, hebu tusome katikati ya mistari mara moja.

Mara baada ya hao Malaika kuondoka, na Sodoma iliteketezwa, Abrahamu na Sara walikwenda safari ndefu hadi chini Gerari. Hiyo ni safari ndefu hasa kwa watu wawili walio wazee. Ipime hiyo kwenye ramani yako. Wao walikwenda kule chini Gerari. Na Sara yupo hapa sasa, nyanya, akiwa na umri wa miaka tisini, akiwa amevaa kofia ndogo ya kuzuia jua, akitetemeka. Na Abrahamu akiwa na sharafa zake ndefu zikiwa zinaning'inia chini. Biblia ilisema, "Wote wawili wamepigwa na umri." Usijaribu kusema wao waliishi maisha marefu zaidi. Na Biblia inasema, "Miili yao wote wawili ilikuwa imekufa, na kupigwa na umri." Na hapa wanakwenda chini Gerari. Na kuna mfalme kijana chini kule aliyeitwa Abimeleki, na yeye alikuwa anamtafuta mpenzi, na yeye alipomwona Sara alimpenda. Je, hilo ni sahihi? Nyanya?

62 "Mbona, wewe ni zaidi ya wote!" Abrahamu alisema, "Wewe ni mzuri wa kutazama." Amina. "Nakuomba umwambie kuwa wewe ni-ni dada yangu." Haleluya! Yeye alikuwa anaonyesha pale kile Yeye alichokuwa anakwenda kufanya kwa Uzao wote wa Abrahamu. Sara alikuwa mzuri wa sura. Abrahamu alikuwa kijana. Naweza kumsikia Abrahamu akisema, "Sara, mpenzi, unajua nini, mvi zinaondoka kwenye nywele zako."

"Abrahamu, hicho kibiongo kinaondoka kisogoni mwako. Unanyooka." Walirejea kwenye kuwa mwanamume kijana na mwanamke kijana. Mungu alionyesha! Loo, jamani!

63 Na Abimeleki alimpenda, na kwenda na kumchukua, na angelimwoa Sara. Naweza kumwona yeye akioga, na kulala akiwa amevaa nguo za kulala, na kuelekeza vidole vyake vya miguu juu, baada ya yeye kuomba, na kusema, "Kesho, nitamuoa yule mzuri wa umri wa miaka mia." Ni la kuchekesha! "Huyo msichana Mwebrania mzuri! Ee, kaka yake, huyo jamaa mdogo! Na Sara ni mzuri iliyoje!"

Na Mungu alimtokea katika ndoto, na kusema, "Wewe ni kama mtu aliyekufa."

Akasema, "Bwana, ni kwa nini hivyo?"

Yeye Bwana akasema, "Huyo ni mke wa mtu."

Abimeleki akasema, "Wewe unajua uaminifu wa moyo wangu, Bwana. Sara alisema, 'Yule ni kaka yangu.' Na Abrahamu alisema, 'Ni dada yangu.'"

Yeye Bwana akasema, "Mimi najua uaminifu wa moyo wako, hiyo ndiyo sababu nilikuzuia kunitenda dhambi Mimi." Lakini sikilizeni! "Lakini wewe ni kama aliyekufa, na taifa lako lote limekwisha. Mume wake ni nabii Wangu. Mimi sijali wewe ni mtakatifu

iliyoje, unaomba kiasi gani, sitasikia maombi yako. Lakini mume wake ni nabii! Nenda, na umrudishe mke wake na yeye akuombee. Kama hutafanya hivyo, utakufa." Haleluya!

64 Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akiwaandaa Sara na Abrahamu ili kupokea mwana wa ahadi. Ikionyesha kuwa jambo linalofuata baada ya udhihirisho wa huyu Malaika wa Mungu, Roho Mtakatifu akionyesha ishara Yake ya mwisho, jambo linalofuata, huu wa kufa unachukua kutokufa na tunachukuliwa juu hewani ili kukutana na Mwana wa ahadi, Mzao wa kifalme wa Abrahamu. Utukufu kwa Mungu! Haleluya! "Kwani tutabadilika katika kitambo kifupi kufumba na kufumbua, nasi tutachukuliwa juu pamoja ili kukutana na Yeye hewani. Hivyo tutakuwa pamoja na Yeye, Mwana wa ahadi." Haleluya!

65 Ee, sitafikia…Nita…Huenda kesho jioni nitaifikia sura ya 22, unaona.

Ee, nalipenda hilo, sivyo nanyi? Ninafurahi sana, mambo haya yote! Biblia imejaa tu hivi vito vya neema. Ichukue tu na uvichukue, ondoa uchafu kwenye hiyo na uvitazame. Kila kimojawapo kunamuwakilisha Yesu Kristo, kila mtu, kwani ndani Yake hukaa utimilifu wa Mungu. Ndani Yake kila kitu kinamwelekea Yeye. Kila kitu kutoka kwenye Agano la Kale kinaelekeza msalabani; na kilicho katika Agano Jipya, kinaelekeza nyuma msalabani. Hilo ni sahihi. Yote yako pale. Loo!

Kibarikiwe kifungo kinachofunga
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa nia ya udugu
Ni kama huo wa juu.

Ninampenda Yeye iliyoje! Nataka kumwona Yeye iliyoje! Ninatamani iliyoje na kusubiri kubadilishwa kwa huu mwili wa kale uliochoka, uliochubuliwa, uliovunjika moyo, mwili uliodhoofika utakaobadilika katika mojawapo ya hizi asubuhi! Tarumbeta italia na wafu katika Kristo watafufuka. Tutapaa juu pamoja nao, ili kukutana na Bwana hewani.

66 Jinsi yule Rebeka, alivyompa huyo ngamia maji katika kupoa kwa jioni. Eliezeri hakumpata yeye asubuhi. Kamwe yeye hakumpata wakati wa alasiri; alimpata katika nuru ya jioni. "Kutakuweko Nuru wakati wa jioni!" Sawa! Hapo ndipo yeye alipompata. Rebeka alifunika uso wake kwa shela. Yeye hakuwa na kichwa; yeye alikuwa anakwenda kwa kichwa chake. Amina. Mwanamke, ni asili yake, ya mwanamke, kujisalimisha kwa mwanamume. Na ni asili ya kanisa kujisalimisha kwa Kristo, kujisalimisha, kwenye nia Yake. Jisalimishe tu! Yeye hana kufikiri kwake mwenyewe; yeye huchukua Neno Lake, siyo la mtu mwingine. Kama Hawa angelikuwa amefanya hilo, kamwe tusingelikufa; lakini yeye alisikiliza hoja. Lakini Bibiarusi halisi wa Kristo huchukua Uongozi wa Kristo, lile Neno, na huliamini Neno la Mungu pekee. Huyo ni Bibiarusi halisi aliyerejeshwa. Haleluya! Wakati umekaribia, marafiki, tumechelewa kuliko mnavyofikiri. Tuko kwenye wakati wa jioni. Roho Mtakatifu yupo hapa jioni hii. Mimi najua hili ni kundi dogo kidogo.

67 Ungefikiri, "Ee, kama kitu kama hicho kingetokea, Mungu angelidhihirisha hilo huko katika Rumi, kwa maskofu na kwa mapapa. Yeye angelikuja kwa askofu wa Methodisti. Yeye angelikwenda seminari ya Baptisti. Yeye ange…" Naam, hilo ndilo unalofikiria. Lakini kamwe Yeye hakufanya hilo namna hiyo.

Yeye anakuja kwa wanyenyekevu wa mioyo, hao wanaomtazamia Yeye. Na Yeye yupo hapa jioni hii, Roho Mtakatifu, Mungu, Malaika yule yule; hapa mbele ya wanasayansi, akithibitisha, Yeye yupo pale pamoja na picha Yake iliyopigwa. George J. Lacy, mkuu wa nyaraka za alama za vidole wa FBI, yeye alisema, "Nuru iliigonga lensi." Yeye alisema, "Bw. Branham, nimekwishakusema mara nyingi kuwa hilo lilikuwa saikolojia, kwamba ulikuwa unasoma akili za hao watu. Lakini" kasema, "jicho la hii kamera haliwezi kuchukua saikolojia. Ile Nuru iligonga lensi. Hiyo ilikuwa pale!" Hiyo iko pale . Mojawapo inaning'inia katika Washington D.C., ikiwa na haki ya kutoinakili, "Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha kisanyansi na kuthibitishwa.

68 Kwa nini? Kama nikifa jioni hii, kama kamwe sitaiingia hii madhabahu kesho usiku, maneno yangu ni ile Kweli. Kwa sababu, siyo maneno yangu, ni Yake. Kamwe sikusema, "mimi mwenyewe." Siyo mimi. Mimi singeweza kufanya chochote. Mimi ni mwanadamu kama ninyi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Lakini Mungu, katika hizi siku za mwisho, aliahidi haya mambo, na ndiyo haya hapa! Hilo ni Neno. Kama ilikuwa ni uzushi fulani, huenda ikawa tofauti. Lakini hilo ni Neno likithibitisha Neno kwa Neno, lililothibitishwa, kote kwenye Biblia. Lililothibitishwa na wanasayansi. Lililothibitishwa kwa Roho! Lililothibitihswa na kanisa! Mungu miongoni mwetu! Haleluya. Mimi nafurahi

mno hilo. Je, hamfurahii jioni iliyopita, mlisimama na kufanya huo msimamo! Je, hilo liliwafanya mjisikie vizuri? Siku zote litafanya hivyo, unaposimama kwa ajili ya Neno la Mungu. Simama kwa ajili ya Kristo! Usilionee haya hilo.

69 Hebu tuombe. Je, kuna yeyote hapa jioni hii angelipenda kuinua mkono wake juu kwa kitambo kidogo tu sasa, na aseme, "Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi yako. Mimi nita, ninatamani sana kuwa mmoja wa huo Uzao wa Abrahamu. Mimi-mimi sitaki kuikosa Mbingu. Omba, Ndugu Branham. Siku zote chini katika moyo wangu nilijisikia kama kwamba kulikuweko na kitu fulani nilichokiendea. Kamwe sijaweza kukipata. Niombee, Ndugu Branham, kwamba Mungu atanipa hicho"? Mungu akubariki. Itazame tu hiyo mikono, kila mahali, ikiinuliwa juu.

Vipi juu ya huko roshani? Sasa, kumbukeni, Mungu ni mkuu tu katika roshani kama Yeye alivyo chini hapa.

Je, wewe ni mwaminifu hasa, unalimaanisha hilo? Inua juu mkono wako. Mungu akubariki. Ninatazama tu kwa kitambo kidogo. Endelea kuomba tu, endeleeni kuinamisha vichwa vyenu.

Mwenye dhambi ndani hapa jioni hii angelitaka kuinua mkono wao, aseme, "Nikumbuke, Bwana. Simwinulii mkono wangu yule mhubiri; ninainua juu mkono wangu Kwako. Kwa kweli mimi naamini kuwa Wewe unaishi leo hii, kwamba Wewe kamwe hukufa; kwamba Wewe ulipokufa, ulifufuka tena, ndiyo namaanisha. Na Wewe u hai milele na milele, yule jana, leo, na hata milele na milele. Ninainua juu mkono wangu Kwako, kwa sababu naamini Wewe uko hapa"? Inua juu mkono wako, useme, "Nikumbuke, Bwana." Endelea tu kuomba. Iweni na imani kwa Mungu.

Aliyerudi nyuma, basi? Mungu akubariki. Yeye anaiona mikono yako.

70 Baba yetu wa Mbinguni, unaona hiyo mikono. Unajua kile kilicho nyuma ya hiyo. Wewe ulisema, "Mpanzi alitoka kwenda kupanda Mbegu. Baadhi ziliangukа kando ya njia, hazikustawi; baadhi zilianguka juu ya ardhi ya mawemawe; baadhi kwenye miiba; baadhi zilikwenda katika mia mia." Yule mpanzi yeye aliwajibika tu kupanda Mbegu. Hebu Roho Mtakatifu adake hiyo Mbegu sasa hivi. Bwana. Mimi naamini, Bwana.

Hakuna mtu anayejua ni lini Wewe unakuja. Sisi hatukujua hilo. Wewe ulisema, "Hata Malaika wasingejua; ni Baba tu pekee." Yeye alidai kuwa Yeye hakujua. "Ni Baba tu pekee." Sasa, Baba, naomba kwamba kama kuna hao ndani hapa walioinua mikono yao juu. Naamini walimaanisha hilo. Kuna Kitu Fulani nyuma yao, ambacho, Roho, aliyewaambia wainue mikono yao juu, nao wakafanya hivyo. Wao ni waaminifu. Huenda hii ni mara yao ya kwanza Wewe kuwahi kunena nao, na labda mara ya mwisho. Huenda Wewe utawanenea mara nyingine, na kamwe usiwanenee kwa mara nyingine. Mimi sijui. Lakini, Baba wa Mbinguni, naomba kwamba utatujalia wokovu kwa kila mmoja anayeamini.

71 Hebu Jina Lako Takatifu liletwe katika heshima sana mbele za watu. Hebu upendo Wako usambae kote katika kila moyo kwa njia ya Roho Mtakatifu. Bariki hawa ndugu wahudumu, Bwana. Hawa watu wa thamani hapa ambao, katikati ya mapambano, hao wametukaribisha, hata hivyo. Bariki hawa watu wanaohudhuria.

Mimi simaanishi kuwa na kupenda makuu, simaanishi kuwa tofauti, Bwana; ni kuwa mkweli tu. Na hicho ndicho kitu pekee ambacho Wewe utakitambua, ni huo ukweli ulio ndani ya mtu, kwani Wewe ndiyo ile Kweli. Sikia sasa, Baba, naomba. Wajalie hao jioni hii kwamba wengi wao hapa, ambao huenda hawakuinua mikono yao, wataokoka, hata hivyo. Tujalie hilo, katika Jina la Yesu. Amina.

72 Sasa tunapoketi kwa heshima sana kwa kitambo kidogo tu, naamini tumechelewa kidogo kuwa na msitari wa maombi, lakini tutakuwa nao. Kila mtu, unapo…ninyi, kama unayo kadi, usihikilie kadi yako. Kama huna kadi, uchukue moja. Tuna…Kama inatupasa kukaa hapa siku tano za ziada, tunakwenda kuomba kwa ajili ya kila mmoja wao. Hilo ni sahihi.

Ninajaribu tu kuleta Ujumbe kwa watu. Najaribu kuwafanya ili mwone hilo kuu… Kama ukiponywa; labda kama utaishi kirefu vya kutosha, utaugua tena wakati fulani. Lakini kama utaokolewa, unakuwa na Uzima wa Milele. Unaona? Unaweza kuponywa, na kuenenda katika njia yako na upoteze wokovu wako…ungeweza kupoteza uhai wako, ndiyo namaanisha; lakini unapokuwa umeokolewa, basi unakuwa na Uzima wa Milele, kamwe hutaugua.

73 Sijui kama mlielewa jioni hii kile nilichokuwa ninakizungumzia, kuwa Mungu aliwatokea Abrahamu na Sara, kule, na akawapa ile ishara ya mwisho, yule Malaika, kwamba kabla ya maangamizi kuja na kupewa mwana wa ahadi. Kwa Kanisa, ishara hiyo hiyo, Mwana wa ahadi alikuwa anakuja. Kwa ulimwengu, ilikuwa ni maangamizi. Sasa, kile Yeye alichofanya kwa Abrahamu na hao ilikuwa ni mifano.

Yesu alikuja duniani, ule Uzao wa kifalme wa Abrahamu, na akatenda ishara ile ile. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa hivyo, waseme, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." -Mh.] Hakika. Nao waliikataa hiyo. Je, hilo ni sahihi?

Sasa, kamwe Yeye hakufanya hilo kwa Mataifa, kwa sababu ule Uzao wa kifalme haukuwa umetokea, Kanisa halikuwa limezaliwa bado. Lakini Kanisa lilipozaliwa, na sasa limekuwa na miaka elfu mbili, penye tu … Kumbukeni, hilo lilikuwa penye kufunga kusubiri kwa Abrahamu. Hilo lilikuwa penye kufunga kwa uzao wa asili kumsubiri Masihi, kwa sababu Masihi alikuwa pale.

74 Huku ni kufungwa kusubiri kuja kwa Uzao wa kifalme. Yeye yupo hapa, kutokea kwa Kristo. Je, uliwahi kugawa … Kuna mahali katika Biblia, unajua, sina muda wa kuingia katika hilo, panasema, "kuonekana kwa Kristo," na ndipo "Kuja kwa Kristo." Hayo ni mambo mawili tofauti, kabisa, kule "kuonekana" na kule "Kuja." Yeye anatokea sasa, akitenda kazi pamoja nasi katika umbo la Roho Mtakatifu, akilifanya hilo kamilifu tu, Kanisa. Inapasa liwe.

Kama vile ukiwa na dola mfukoni mwako, itoe nje na uitazame. Upande mmoja ni lakiri ya Amerika; kwenye upande mwingine ni lakiri ya Kimisri, piramidi ikiwa na jiwe la kifuniko juu yake, kama jicho linalotazama. Na mbona dola ya Amerika iwekwe chini pale, "Ile lakiri kuu!"? Inaonekana kama kwamba lakiri ya Amerika ingelikuwa lakiri kuu hapa. Lakini Serikali ya Amerika inatambua hilo ikiwa wao wanataka hilo au la, ile lakiri kuu.

Tazama ile piramidi inavyojitengeneza, Kanisa. Kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na ndipo hilo inapasa linolewe wakati…Lile Jiwe la kifuniko kamwe halijaja kwenye piramidi, Hilo lilikataliwa, kama tu Jiwe kuu la pembeni. Sasa, lakini hilo Jiwe kuu la pembeni litakapokuja…Mimi nimekwenda kwenye piramidi; imelinganishwa tu kikamilifu mno, hungeweza kupitisha wembe kati yake, pale simenti ilipo. Na Kanisa litakapokuja, hiyo ni…Kristo atakapokuja kulipokea Kanisa Lake, Kanisa litakuwa na huduma kama hiyo tu kabisa, na kupitia hiyo neema, litainua hilo jambo lote, ndipo liende. Kuja kwa Jiwe kuu la pembeni. Likilia, "Neema, kwa Bwana."

75 Ninalo jambo fulani akilini mwangu. Haleluya! Mungu wetu bado ndiye aliye Mungu. Yeye hufunua siri Zake kwa watumishi Wake. Nilinena juu ya yule Malaika aliyepiga kisogo kwenye hema, naye alikuwa amepiga hema kisogo, na kusema kile Sara alichokuwa akiwazia huko ndani. Nabashiri kuwa yule Malaika yupo hapa sasa, Roho Mtakatifu, ile ile Nguzo ya Moto, Yule yule Ambaye alikuwa ndani Yake Kristo. Ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Hiyo Nguzo ya Moto ilifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Yeye alisema, "Mimi natoka kwa Mungu, nakwenda kwa Mungu."

Baada ya kifo Chake, kuzikwa, kufufuka, kupaa, Yeye alikutana na Sauli njiani chini kwenda Dameski. Na Nuru ilimgonga na kumwangusha chini. Na yeye akasema, "Bwana, Bwana!"

Yeye Bwana akasema, "Sauli, Sauli," kwanza, "Wewe ni … Kwa nini unanitesa?"

Kasema, "Wewe ni Nani, Bwana?"

Yeye akasema, "Mimi ni Yesu." Alirejea nyuma!

76 Yeye yupo hapa jioni hii, aliyethibitishwa na Kanisa Lake, kisayansi na yote! Ee, marafiki, kwa nini tumekuwa wazito wa kuelewa hivyo? Kwa nini tunaketi tukiwa tumeinamia kwa ajili ya uchovu hivyo? Hebu yule-hebu yule Mungu aliyenena lile Neno, hebu yule Mungu ambaye…Kama Elisha alivyosema, aliyerejea na sehemu maradufu ya Eliya, alikunja lile joho, na kusema, "Mungu wa Eliya yuko wapi?" Hebu huyo Mungu aliyeliandika Neno, athibitishe hilo Neno! Kama hili ni Neno Lake, hebu Yeye asimamie Hilo! Yeye aliahidi kufanya hilo. Yeye atafanya hilo kama tutaliamini.

Sasa hebu mimi nilifanye hilo lijulikane kwa uwazi. Mimi siyo huyo Mtu. Mimi ni mtumishi kwa huyo Mtu. Na wewe pia, kama wewe ni Mzao wa Abrahamu.

77 Lakini mimi kwa kuhubiri, Neno Lake, na kusimama katika siku ambapo kila

dhehebu limeniacha, mashirika ya dini yananitupa nje toka mahali hadi mahali. Na ni ndugu wa thamani tu ambao wako katika hayo mashirika ya dini, wanaoiona Nuru, watalishikilia Hilo pasipo kujali kile ambacho makao makuu yanachosema. Mungu awabariki watu kama hao. Mungu awabariki wanawake na mwanamume waliosimama jioni iliyopita. Mimi nitawafanyia nini? Niombeni kitu fulani. Niombeni kitu cha kufanya, nitafanya kitu chochote kwa ajili yenu. Ninyi ni watu wa Mungu. Mwanamume yeyote au mwanamke yeyote atakayeweka msimamo kama huo, katikati ya mapambano, ninayo heshima kwake.

78 Sasa kama yule Malaika…Kama Neno la Yesu Kristo limebashiriwa, kuwa kabla tu ya kuja kwa Mwana adamu, kuwa kitu kile kile kilichotukia kule Sodoma kingetukia kwenye Kanisa, hebu Yeye aje kwenye sehemu ya tukio.

Nitawageuzia mgongo wangu. Inamisha kichwa chako uombe. Kwa vyovyote ningesema hili kama sikusikia kuongozwa kufanya hilo. Nitakuwa mpumbavu kwa kutoa tamshi kama hili. Lakini, kwa kuamini katika Kristo Mwana wa Mungu, tukiamini kuwa Yeye ni Neno! Na Neno linafanyika kuwa katika mwili wetu, tunapolichukua Neno, kwa sababu hiyo ni ahadi Yake, "Nitakuwa ndani yenu hadi mwisho wa ulimwengu, na matendo niyatendayo nanyi mtayatenda pia."

79 Nimegeuzia kusanyiko mgongo wangu, Baba wa Mbinguni, kwamba nimewahubiria kwenye huu Ujumbe. Nakuomba Mungu, hebu hilo lijulikane kuwa Wewe bado ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu, na Wewe bado ni Yehova Mungu. Wewe ni yule jana, leo, na hata milele na milele. Na ilikuwa ni Wewe kule ukizungumza na Abrahamu siku ile kwenye hema. Ilikuwa ni Wewe ambaye uliweza kutambua kile yule mwanamke alichokuwa akiwaza ndani ya hema, na ukamwambia. Na wakatu huo huo, yeye akikana hilo, Wewe ungeliweza kuchukua uhai wake, lakini yeye alikuwa sehemu ya Abrahamu, bibiarusi wake. Bwana, Wewe ungelichukua uhai wetu, kwa kutokuamini kwetu, lakini sisi ni sehemu ya Kristo. Usingeliweza kuchukua, kumchukua Sara pasipo kumwumiza Abrahamu. Na huwezi kulichukua Kanisa pa-pasipo kumwumiza Kristo. Nisaidie, Bwana. Mimi sina elimu. Mimi tu ni…Bwana, mimi sina chochote, bali kukuamini Wewe tu. Nami naamini. Nisaidie hilo, Bwana.

80 [Dada fulani ananena katika lugha nyingine. Dada mwingine anatoa fasiri-Mh.] Amina. Shukrani na ziwe kwa Mungu aliye hai. Sasa, Yeye yupo hapa. Uwe mnyenyekevu, heshima.

Unaweza kuinua kichwa chako kama unataka. Sasa siyo tu…Unaona, Biblia inasema kuwa kunena kwa lugha ni kufaidi mwenyewe, isipokuwa pawepo na fasiri. Na kama hiyo fasiri, huo ni unabii kwa Kanisa. Na ninavyoelewa hiyo fasiri basi, ilikuwa ni "Mwamini Bwana, kuwa ni Yeye aliyetuma Neno." Na basi kamwe sikuja katika jina langu mwenyewe, nilikuja katika Jina Lake. Na Yeye angelitenda matendo Yake kupitia kwangu basi, kwa kuhubiri Neno Lake na kuthibitisha Neno Lake. Hakika. Mimi naamini hilo. Je, wewe unaamini vivyo hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Ni wangapi wanaamini hilo sasa, kabla Yeye…? Mungu akubariki. Sasa hiyo ndiyo njia ya kwenda, hiyo ndiyo njia. Shikilia hiyo mizania nawe utaona jambo fulani likitukia.

81 Nakwenda kugeuzia kusanyiko mgongo wangu, kwa sababu huyo alikuwa Roho Mtakatifu akilishuhudia tu hilo. Unaona? Iweni imara na kile cha kufanya. Sasa mnaamini nje huko kwenye kusanyiko, mtu fulani. Hakuna tu niwezaye kumwona … Ni wangapi nje huko ni wagonjwa na wanaoteseka, au aliye na kitu fulani kingine ambacho unakiombea, nawe unajua mimi sijui lolote juu yake, inua tu juu mkono wako. Vema, nadhani ni karibu kila mahali. Vema, hebu tuamini tu sasa. Asi, asiondoke hata mmoja, mpe tu…Ni saa nne kasoro dakika kumi na mbili. Nipeni dakika kumi na mbili, mtanipa? Mtu yeyote asiondoke, hata kidogo. Ketini kwa utulivu tu. Wakati mmoja tu, fungua moyo wako.

82 [Ndugu fulani ananena kwa lugha nyingine. Ndugu mwingine anatoa fasiri-Mh.] Amina. Asante, Bwana, asante. Kwa unyenyekevu tunaheshimu hilo kwa moyo wetu wote. Hiyo ni karama ndani ya Kanisa. Iweni katika maombi tu, kwa heshima sana.

Kumbukeni, wao walikuwa wanakwenda vitani wakati mmoja, wao hawakujua jinsi ya kukabiliana na hii vita kuu. Daudi alikuwa amesimama pale, na akagawana nao kipande cha nyama na gudulia la divai. Lakini Roho alishuka juu ya mtu mmoja, na yeye akatabiri na kuwaambia ni wapi pa kukutana na adui, na ilikuwa hivyo.

Tunakabilia na vita kuu, ndugu. Na tumesimama katika vita kuu sasa hivi. Roho

ameshuka na, juu ya mtu fulani, na amewaambia ni nini tu cha kufanya, "kuamini." Yeye anajaribu kuondoa akili zenu mbali na kuwa na mimi. Unaona? Baadhi yenu lazima wanafikiri kuwa ni Ndugu Branham anayejaribu kufanya jambo fulani. Siyo mimi; ni Yeye. Mimi tu…Karama ni kujitoa tu wewe mwenyewe, kama kuvuta gia wewe mwenyewe. Kama tu hiki kipaza sauti, unakiwasha, kitu fulani inapasa kinene kupitia hicho. Ni gia ndogo tu ninayowasha, kitu kidogo. Roho Mtakatifu! Mimi siwashi hilo; Yeye analiwasha. Na ndipo Yeye ananena; siyo mimi. Sasa iweni wanyenyekevu na kuamini, kila mmoja wenu, na ombeni tu.

83 Sasa, kila mmoja anajua kuwa Biblia ilisema kuwa "Yesu Kristo sasa hivi ni Kuhami Mkuu ambaye anaweza kuguswa na hisia za udhaifu wetu." Kama hilo ni sahihi, hebu kusanyiko liseme, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina"-Mh.] Je, Yeye ni yule yule Kuhani Mkuu? Semeni, "Amina." ["Amina."] Kama Yeye ni yule yule Kuhami Mkuu, Yeye atatenda kwa njia ile ile. Je, hilo ni sahihi? ["Amina."] Amina. Sasa mtafanya nini?

Sasa, kunigusa mimi, lisingeleta tofauti yoyote; mimi ni mwanadamu. Lakini kumgusa Yeye, basi Yeye ni Roho Mtakatifu aliye ndani hapa, basi Yeye anajibu na hutumia midomo ya mwanadamu. Kwa sababu, Yeye ni Mzabibu, sisi ni matawi; Yeye hazai matunda, Yeye hulipa tu tawi nguvu.

Yaani, geukeni tu nyuma yangu, ili mweze kuona hayo mambo niliyosema...

84 Sasa hawa wahudumu hapa jukwaani, wanaomba. Mnaweza kunitazama kama mnataka. Hilo ni sawa. Ili tu kuona, mnaweza kujua kuwa wao tu…Bila shaka, wewe ni mchunga kondoo, wewe ndiye unayewachunga hawa kondoo. Hivyo, ili muweze kujua. Na nataka mniombee, ndugu. Bila shaka, mnaona kile mimi nilicho? Mimi namwakilisha yule yule Kristo mnayemtumikia. Na mimi ni ndugu yenu, raia mwenzenu wa ule Ufalme pamoja nanyi ndugu. Nami nipo tu hapa…

Unaona, sasa, sasa hivi hilo Neno nililohubiri, unaona, liko hatarini. Hivi sasa, kushindwa, hilo ndilo Shetani angetaka kuona. Hilo ndilo tu yeye analotazamia. Lakini Mungu hashindwi. Iweni wanyenyekevu tu.

85 Sasa nikiwa nimewageuzia mgongo wangu, nataka mtu fulani…Hebu nigeuze huo, ni kote. Hebu nigeukie sehemu *hii*, kwanza, na ndipo nitakuja huko kwenye sehemu ile *nyingine*. Sasa mtu fulani nyuma upande huu; kuna wengi mno, kama, wakiomba. Turudi katika upande huu, mtu fulani akiwa anaomba nyuma hapa sasa, anayetaka kumwamini Mungu. Amini tu kwa moyo wako wote, turudi hapa mahali fulani.

Sasa, Baba wa Mbinguni, mimi-mimi nakushukuru katika jumbe Zako, kila kitu ulichofanya. Sasa nisaidie, Bwana. Nina-nina…kwa imani, nakuamini Wewe, Neno Lako. Naamini huyo alikuwa Roho Wako aliyeniita kufanya hili. Sasa hebu lijulikane kuwa mimi nimenena ile Kweli. Nimeshuhudia juu Yako, sasa shuhudia, Bwana, kuwa nilisema ile Kweli. Naomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

86 [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine-Mh.]

Baba Mungu, tunasubiri fasiri ya hilo. Wewe ulisema, katika Biblia, kungekuwako "mielekeo mitatu," na huo ni wa tatu. Sasa sisi-sisi tunaomba kwamba-kwamba utamjulisha hilo mtu fulani aliye na hizo karama za fasiri. Naliacha hilo kwako, katika Jina la Kristo.

[Ndugu fulani anatoa unabii-Mh.] Asante, Bwana.

Sasa, huo ulikuwa unabii, siyo fasiri. Unaona, yeye alisema mengi kuliko yale aliyosema huyo mwanamke. Kuna fasiri inayokuja. Unaona, huyo mwanamume alikuwa...

[Ndugu fulani anatoa fasiri-Mh.] Amina. Asante, Bwana.

Moja kwa moja nyuma yangu... [Dada fulani katika kusanyiko anaanza kuomba-Mh.] Mungu, mjalie baraka huyo mwanamke, hicho anacholilia. Awe tu na…

Sasa uwe mnyenyekevu hasa sasa, na amini hilo kwa moyo wako wote. Sasa, kwa njia ya Roho Mtakatifu, najaribu kulileta Neno ambalo nimehubiri, ambalo Yeye ameshuhudia kuwa hilo litatukia. Sasa amini kwa moyo wako wote.

87 Kuna mtu fulani aliyesimama mbele yangu, ambaye amekaa nyuma yangu. Naye ni mwanamke. Na yeye anaumwa na tatizo la moyo. Naye ana aleji inayomsumbua. Yeye yupo tu nyuma yangu. Kama huyo mwanamke hajasimama bado…Kusanyiko likiwa

linamtazama; mimi nimefumba macho yangu. Yeye pia ana hofu kuhusika juu ya mpendwa, ambaye, mume wake aliyeketi kando yake; yeye amepooza, na mkongojo wa kutembea. Jina la huyo mwanamke ni Bibi Brumley. Amini kwa moyo wako wote. Simamana upokee kile ulichoomba, nawe utapata kile ulichoomba. Simama wima kwa miguu yako. Je, amesimama? [Kusanyiko linasema, "Ndiyo."-Mh.]

Mungu akubariki. Mimi simfahamu huyo mwanamke, kamwe sikuwahi kumwona katika maisha yangu. Sisi ni wageni sisi kwa sisi? Kuna…[Huyo mwanamke anasema, "Ndiyo."-Mh.] Sasa waulize, nenda na uwaulize kama hilo ni sahihi. Sasa kama huyo siyo Mungu yule yule aliyekuwa chini mbele ya Sodoma, mimi sijui ni nani huyo.

88 Mtu fulani mwingine katika sehemu hii amini sasa kwa moyo wako wote, Bwana Yesu. Kuna mwanamke aliyeketi hapa hapa nyuma yangu. Yeye anayo shauku ya kina. Yeye anamwomba Mungu ampe kitu fulani. Ni mtoto, anaomba, kwa ajili ya mtoto. Yeye yupo hapa hapa nyuma yangu. Bibi Holm, inuka na umwamini Bwana Mungu. Na kama utaamini hilo kwa moyo wako wote, unaweza kuwa na mtoto unayeombea.

Mwanamke fulani anaingia ndani, na yeye ni kiwete. Yeye ameketi katika kiti chenye magurudumu. Yeye yuko nyuma yangu. Yeye hatokei sehemu hii ya nchi. Anatokea-anatokea Sacramento, Sacramento ya kaskazini. Yeye amekuwa mgonjwa sana. Madaktari hawawezi kumsaidia. Yeye amekuwa hospitalini, yeye amekuwa na upasuaji mara kadhaa. Yeye ana tatizo la figo, tatizo la mifupa yake. Ana wasiwasi tu, hadi anakuwa na matatizo ya ziada. Yeye ana hali mbaya sana. Bibi Bealer, pale, shikilia mkono wako juu na uamini kuwa Bwana Yesu…na ufanyike…Mungu akubariki.

89 Je, unaamini? Mungu bado anaishi na kutawala. Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote!

Hapa kuna mwanamke mdogo. Namtazama yeye akiwa ameketi hapa. Yeye anaumwa na tatizo la utumbo mkubwa. Jina lake, mimi simfahamu yeye. Lakini wewe unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani, bibiye? Bibi Berglund. Amini kwa moyo wako wote, na unaweza kufanyika kuwa mzima. Amini.

Hapa kuna bibiye akiwa ameketi papa hapa, akiombea rafiki aliyevunjiwa chombo. Amini kwa moyo wako wote, unaweza kupata ulichoomba.

Kuna bibiye aliyeketi pale akiumwa kichwa. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kufanywa kuwa mzima. Usitie shaka hilo. Amini tu. Kama Yeye siyo Mungu yule yule, mimi sijui Yeye ni nani. Yeye yupo hapa ku-ku, kama utakubali hilo na kuliamini.

90 [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine-Mh.] Amina. Bwana asifiwe.

Je, hamwezi kutambua mko Uweponi mwa Mungu? Mfanye hilo. Sasa nafikiri kile ambacho tungefanya sasa hivi, baada ya Roho kunena, "Njooni Kwangu, niaminini Mimi, watu Wangu." Nafikiri tunapaswa kusitisha kwa ajili ya wito wa madhabahuni hivi sasa, na tuwaruhusu hao ambao hawamjui Kristo kuja juu kwenye madhabahu hapa na kumpokea Yeye kama Mwokozi wako. Kama hujampokea Roho Mtakatifu, uje, pia, kumpokea Roho Mtakatifu, kwa sababu ni hilo tu linalokwenda kutukia. Je, hamtakuja sasa tunapoimba; mtu fulani anakwenda kuongoza uimbaji. Roho Mtakatifu amekuwa akinena. Mungu akubariki dada. Hilo ni sawa. Mtu fulani mwingine atoke moja kwa moja pamoja na bibiye hapa. Njoo moja kwa moja juu kama unalo hilo…Mungu akubariki dada. Katika Uwepo pale ambapo Biblia, Neno, uthibitisho, karama, kila kitu kikitenda kazi, je, hilo si la ajabu sasa hivi? Njoo moja kwa moja juu madhabahuni. Shuka chini kutoka roshani. Wewe usiye na Mungu, usiyejazwa na Roho, njoo sasa tunapoimba.

> Yesu anapita njia hii,
> Anapita tu njia hii, leo,
> Yesu anapita njia hii,
> Yeye anapita njia hii leo.
> Yesu anapita njia hii, (Je, hutakuja sasa Yeye
> anapopita, Roho Wake anatembea, akisema,
> "Njoo"?)…leo,
>
> Yesu anapita njia hii,
> Yeye anapita njia hii leo.

91 Je, hutakuja wakati Yeye anapita? Tazama kile Yeye anachofanya miongoni mwenu,

akidhihirisha kuwa Ndiye Yeye yule. Tembea utoke moja kwa moja; kila nafsi ambayo haimjui Yeye, isiyozaliwa mara ya pili. Je, hutakuja sasa ili kumtafuta Yeye? Kumbuka, yule yule Roho Mtakatifu anakujua wewe. "…njia leo."

Yesu anapita njia hii,
Anapita njia hii, leo,
Ee, Yesu anapita njia hii,
Yeye anapita njia hii leo.

Sasa hebu kila nafsi ije sasa ile ambayo haimjui Mungu, ile ambayo haina uhakika na msimamo wako. Uje chini. Usi-usiwe … Usiwe na dhana ya kiakili juu ya hilo, ndugu, dada. Usifanye hilo. Unaweza ukawa umefanya namna yoyote ya msisimko. Huenda ukawa na damu mkononi mwako, usoni pako, unaweza ukawa umekuwa na mitetemeko, na kadahalika. Hakuna chochote ninachopingana nacho, sasa, hilo ni sawa. Wewe huenda umenena kwa lugha, unaweza ukawa umecheza katika Roho, na bado upotee. Hilo ni sahihi. Inapasa uwe Uzima uliozaliwa ndani yako, unaochukua hili Neno na kulifanya liwe hai tena. Unaona, Kristo ni Neno. Na kama huna imani bado ya kuingia katika hilo Neno na kuliamini Hilo, je, hutakuja sasa?

92 Kama Kanisa la Mungu, kama ambavyo Nuru za jioni zinaanza kung'aa, na huo-huo mti unaiva; Mungu alisema Yeye angeliurejesha huo mti, huo huo mti wa pentekoste, aina ile ile ya Imani, kila kitu kile kile walichokuwa nacho, huo mti utarejeshwa tena; pasipo dhehebu, pasipo kitu chochote, utakuja katika nguvu rahisi za Roho Mtakatifu, akifundisha Biblia kabisa tu kama ambavyo Yeye alifanya hilo. Tunaahidiwa mmoja katika siku za mwisho, unajua, angekuja na kurejesha hiyo Imani. Hivyo mimi naamini Yeye yupo hapa jioni hii, katika umbo la Roho Mtakatifu. Njoo sasa, tunapoimba tena, hivyo tutakuwa na hakika tumemaliza hilo.

93 Sasa kumbukeni kama hizi roho … Ninyi watu Wapentekoste hakika mnaamini karama zenu za lugha na fasiri! Kama hamtaamini kile Yeye alichofanya *hapa*, basi aminini lugha na fasiri zenu, za kuwaita madhabahuni. Hebu kila mmoja aje. Kama mnaona hilo likitenda kazi, hili likitenda kazi, Mungu akitenda kazi, mbona, huyo ni Mungu! Vipi zaidi, hapa kuna Neno hapa likithibitisha Hilo, likisema kuwa Hilo ni ile Kweli. Njoo. Mara moja nyingine sasa, na uje sasa.

Yesu anapita njia hii,
Leo, leo,
Yesu anapita njia hii,
Yeye anapita njia hii leo.

94 Sasa hebu hao wanaomwamini Mungu, wahudumu watakatifu halisi na-na watumishi wa Kristo, njooni, mkitoka hali tunapoimba tena sasa. Msogee karibu na madhabahu, kuzunguka hawa hapa. Na hebu tuombe pamoja nao, kwa pamoja. Njooni. Je, hamji karibu? Siwezi kuwafikia hao, kila mmoja, kwa mikono yangu. Nataka mje. Baadhi yenu ndugu mnaohudumu waendeeni mongoni mwao chini pale sasa, ili muweze kuwagusa na muweke mikono yenu juu yao. Vema. Ninyi mnaomjua Mungu, njooni, mkitembea juu hapa, baadhi yenu wanawake pamoja na hawa wanawake, ninyi wanaume na hawa wanaume. Sogeeni juu hapa sasa. Huu ni utaratibu wa Mungu. Tembeeni kuja juu sasa, ninyi watu. Hilo, hilo ndilo lenyewe, huo ndio wakati. Baadhi yenu akina mama wacha Mungu na baadhi yenu ndugu wacha Mungu, tembeeni kuja hapa sasa ili muweze kuweka mikono yenu juu yao, katika uthibitisho, mkiweka mikono yenu juu yao ili kwamba waweze kumpokea Roho Mtakatifu. Vema. Sasa hilo ndilo jambo lenyewe. Hilo ndilo jambo lenyewe.

95 Sasa, kwa nini mlikuja? Kwa sababu kwamba mnaamini. Mmeshawishika kuwa Mungu yupo katikati yetu. Yeye yupo hapa jioni hii. Yeye yupo hapa akitenda kazi katika ishara kuu na maajabu.

Sogea moja kwa moja karibu, kila mmoja. Sogeeni moja kwa moja ndani ili watu waweze kuwa na nafasi zaidi. Sogeeni moja kwa moja karibu. Kuna wengi zaidi wanaokuja chini kwenye njia kati ya safu za viti, unaona. Sogea karibu.

Ni wangapi katika kusanyiko wanahofia juu ya hawa watu waliosimama hapa sasa, juu ya wokovu wa nafsi zao, inua juu mkono wako. Vema. Hebu sote kwa pamoja sasa, tumwinulie Mungu mikono yetu, na tuombe.

96 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea jioni hii hili kusanyiko tukiwa na Roho

Mtakatifu katikati yetu, akiwepo sasa, akifanya Neno Lake liishi upya tena. Jaza kila moyo, Bwana. Uje katika nguvu za Roho. Tujalie hilo, Bwana. Ondoa kila hofu, kila pepo. Ingia ndani kwa njia ya nguvu za Mungu, na umiliki hizi nafsi. Katika Jina la Yesu Kristo, nawakabidhi Kwako kwa ajili ya utukufu Wako.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*